SportPesa
TZS. 619,207,580
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Donge** nono milioni 10/- ukiiona ndege na rubani aliyepotea

UKURASA 3



**Martinez atia saini mkataba mpya Inter Milan**

UKURASA 22


# Nipashe

Jumamosi Oktoba 30, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580749

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Majaliwa awaonya mawaziri ulevi

UKURASA 2




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akizungumza alipofungua mafunzo ya uongozi kwa Mawaziri na Manaibu Waziri, yaliyoandaliwa na Taasisi ya Uongozi, jijini Dodoma jana. Kulia ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa na Spika mstaafu Anne Makinda. **PICHA: OWM**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**TANZANIA YAISHUKURU WB UTEKELEZAJI MIRADI**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, ameishukuru...

## Kero ya vibali vya NEMC yapatiwa ufumbuzi

UKURASA 3




Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Freeman Mbowe, akishuka kwenye gari kuingia katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, Sinza mkoani Dar es Salaam jana, kusikiliza mashitaka yanayomkabili. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Shahidi adai kuchanganywa na maswali ya Wakili Mallya

• **Adai** fasili ya ugaidi ni utalii... *Endelea ukurasa 2*




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


**MICHEZO** YANGA YATAMBA KUIPOTEZA AZAM UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6



Wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga, wakiwa wamejenga vibanda vyao juu ya mifereji ya maji ya mvua, wakiendelea na shughuli zao kama kawaida katika eneo la Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam jana, licha ya mkuu wa mkoa huo kutoa siku 12 wawe wameshaondoka. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Majaliwa aonya mawaziri ulevi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ameonya matumizi mabaya ya simu za mkononi na unywaji pombe kupita kiasi kwa mawaziri na manaibu wao.

Majaliwa alitoa onyo hilo jana alipokuwa akifungua mafunzo ya uongozi kwa mawaziri na naibu Mawaziri wa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yaliyoandaliwa na Taasisi ya Uongozi.

Alisema moja ya majukumu waliyo nayo viongozi hao ni kuhakikisha siri za serikali zinatunzwa hasa wakati huu wa utandawazi.

"Leo hii unakuta barua ya siri ya serikali inasambazwa kwenye mitandao ya 'facebook' na wahusika wakuu wa kulinda siri hizi ni ninyi. Pia kumeibuka tabia ya viongozi wa serikali kuzima simu zao hali ambayo inawanyima fursa viongozi wakuu wa nchi kutoa maagizo yao kila wanapohitaji kufanya hivyo.

"Ninyi ni wawakilishi wa viongozi wakuu wa nchi, lakini hivi sasa mnazima sana simu usiku wakati mwingine tunataka kutoa maagizo kwenu kwani nyie ndio wawakilishi wetu tunashindwa, hivyo nawaomba msizime simu zenu kama mnaogopa kusumbuliwa na wapigakura basi tafuteni 'line' mbili moja kwa ajili ya wapigakura wenu jimboni" alisema Majaliwa

Kuhusu unywaji pombe, Majaliwa aliwataka viongozi hao kuepuka matumizi ya vilevi kupita kiasi kwa kuwa hali hiyo itawaondolea heshima kwa jamii.

"Wewe kama mtu wa kilaji wakati huu si sahihi kwako kwa nafasi uliyo nayo. Kama unataka kupiga kilaji basi beba nenda nacho nyumbani. Ninyi ndiyo sura ya serikali, mnatakiwa muda wote kuwa 'smart'," alisisitiza.

Pia aliwataka viongozi hao kuepuka matumizi ya walinzi binafsi ambao hawajapewa mafunzo ya kuzingatia maadili ya utumishi wa umma ambao ndio wanaweza kuwa sababu ya siri nyingi za serikali kuvuja.

"Kumekuwa na utaratibu ambao kiongozi anatafuta mlinzi wake binafsi au msadizi wake, ambaye hajapatiwa mafunzo na anakuwa anajua siri zote za waziri au kiongozi. Kutokana na hali hiyo, sasa serikali imeaandaa utaratibu wa kuwaandaa watu hawa kabla ya kuanza kutumiwa na viongozi," alisema.

**AKEMEA RUSHWA**

Licha ya kutoa maonyo hayo, Waziri Mkuu pia aliwaagiza mawaziri na manaibu wao kusimamia taasisi na idara zilizoko chini ya wizara zao kuzingatia utawala bora na kukomesha vitendo vya rushwa, ambavyo ndivyo adui mkubwa wa utawala bora.

"Ninapenda kuwakumbusha kuwa ninyi ni nyenzo muhimu katika utendaji wa serikali, hivyo wazembe, wezi na wabadhirifu walioko chini ya mamlaka zenu, lazima wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za serikali. Kila kiongozi lazima awe makini muda wote," alisema.

Alisema ubadhirifu unatakiwa ushughulikiwe mapema kwa weledi na utaalamu bila kulazimika kusimamisha utekelezaji wa shughuli za serikali kwa muda mrefu na hatua zichukuliwe bila kuoneana haya kama kuna ushahidi wa wazi kabla hata Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) hajakagua au viongozi wa juu kuchukua hatua.

**MCHENGERWA ATIA NENO**

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, alisema lengo la mafunzo hayo ni kukumbushana.

"Mheshimiwa Waziri Mkuu tunashukuru kwa serikali kuona upo umuhimu wa sisi viongozi kupata nafasi hii ya mafunzo, ambayo kwa mara ya mwisho yalifanyika katika serikali ya awamu ya nne. Tunakushukuru kwa niaba ya viongozi wetu wakuu kwa maono yenu ya kutupatia mafunzo haya. Natumai tukitoka hapa hatutakuwa kama tulivyoingia," alisema Mchengerwa

Pia aliagiza wizara, taasisi zote kutenga bajeti kwa ajili ya mafunzo hayo ya Taasisi ya Uongozi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uongozi, Kadari Singo, alisema huu ni mwaka wa saba mafunzo kama hayo kutolewa na mada mbalimbali zitawasilishwa kupitia viongozi umma wastaafu.

"Hadi sasa tumeshatoa mafunzo kwa viongozi 8,000 tumefanya utafiti 60, kuwakutanisha viongozi maarufu 75, kwa ajili ya mahojiano na tumeshafungua maktaba yetu ya vitabu," alisema.

# Shahidi adai kuchanganywa na maswali kesi ya Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

SHAHIDI wa tatu wa Jamhuri, Koplo Hafidh Mohammed, ameibua miguno kwenye Ukumbi wa Mahakama baada ya kudai 'terrorism' ina fasili ya masuala ya kitalii na kuliandika neno 'conspiracy' kuwa 'consiparancy' katika ripoti yake ya kuchunguza bastola.

Hayo yaliibuka jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi wakati mtaalamu huyo wa kuchunguza silaha na milipuko alipotoa ushahidi katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na wenzake watatu.

Shahidi huyo, akijibu maswali ya Wakili John Mallya, alidai ripoti ya uchunguzi aliotoa mahakamani kama kielelezo inazungumzia kesi iliyopo na uzoefu wake wa miaka 10 wa uchunguzi.

Wakili Mallya alitaka atoe tafsiri ya 'terrorist', akajibu kuwa ni ugadi, lakini alipotakiwa kutoa tafsiri ya 'terrorism', akajibu ni masuala ya utalii.

Majibu hayo yaliibua miguno lakini Wakili Mallya aliendelea kumtaka shahidi asome neno 'conspiracy' aliloandika kwenye ripoti yake kwa herufi moja moja.

Shahidi alitaja herufi alizoandika moja baada ya nyingine, likatoka neno 'consiparancy' na alipotakiwa kutaja herufi moja baada ya nyingine alizoandika kumaanisha 'terrorist', alitaja likasomeka neno 'tellolist'.

Alidai wakati anafanya uchunguzi, alikuwa hajui kama kielelezo kinahusiana na kesi ya ugaidi na kichwa cha habari cha ripoti yake kinachohusu ugaidi alikipata kwenye barua iliyomtaka kufanya uchunguzi wa bastola inayodaiwa alikamatwa nayo mshtakiwa wa pili, Adamu Kasekwa.

Wakili Mallya alitaka shahidi aendelee kujibu maswali badala ya kuuliza tena swali, Jaji Tiganga akamtaka ajibu maswali lakini shahidi alijibu kwamba wakili anamchanganya kwa maswali.

Jaji Tiganga alimwambia shahidi asichanganyikiwe badala yake ajibu maswali ya wakili na wasionekane wanalumbana.

Akihojiwa na Wakili Peter Kibatala, shahidi huyo alidai kwenye bastola limeandikwa neno 'Ruge' lakini kwenye risasi hakuna neno hilo.

Hata hivyo, alipotakiwa kusoma kwenye risasi kimeandikwa nini, alidai haoni na alipohojiwa zaidi kuhusu kilichoandikwa, alisoma neno 'Ruge' limeandikwa kwenye risasi pia.

Hata hivyo, maganda mawili ya risasi yanayodaiwa risasi ilitumika kwenye bunduki hiyo ya Ruge, yalikuwa hayana neno 'Ruge'.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Pius Hillar, shahidi huyo alidai kuwa Novemba 25, 2020, akiwa ofisini, alipokea vielelezo kutoka Ofisi ya DCI ambayo ni bastola aina ya Ruge yenye namba A5340 ya mwaka 1995, vilivyopelekwa kwake na askari aliyemtaja kwa jina la Goodluck.

Alidai barua iliyopelekwa ilimtaka achunguze bastola na risasi kuona kama ni nzima na alianza kuchunguza kwa kupima silaha kwenye kifaa maalum.

Hafidh alidai bastola na risasi tatu baada ya kufanya uchunguzi, zilibainika zilikuwa nzima na alipofanya uchunguzi wa kina kwa kupiga risasi mbili kwenye tangi lenye maji, silaha hiyo ilikuwa inafanya kazi vizuri.

Alidai alipomaliza aliandaa ripoti, akafunga vielelezo kwenye bahasha na kupeleka Amali na Novemba 27 mwaka 2020 afande Swila kutoka Ofisi ya DCI alivifuata vielelezo hivyo.

Shahidi aliomba mahakama ipokee ripoti ya uchunguzi kama kielelezo namba mbili upande wa Jamhuri. Mawakili wa utetezi walipotakiwa kusema kama wanapinga au la, walidai hawana pingamizi.

Mahakama ilipokea kielelezo hicho na kuita P2, kumaanisha kielelezo namba mbili cha upande wa Jamhuri.

Shahidi alitoa bahasha alizotunza bastola, risasi, vichwa vya risasi na maganda yake, akaomba pia vipokewe na mahakama kama kielelezo katika shauri hilo.

Upande wa utetezi kwa mara nyingine hawakuwa na pingamizi. Mahakama ilipokea vielelezo hivyo ambavyo ni bastola namba A5340 ikapewa P3, risasi moja nzima ikawa P4 na maganda ya risasi mbili alizopiga kwenye maji ikawa P4.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Halfani Bwire, Adamu Kasekwa na Mohammed Ling'wenya ambao wanashtakiwa kwa mashtaka sita, ikiwamo kula njama kufanya vitendo vya kigaidi kati ya Mei Mosi na Agosti 5, mwaka 2020.

HABARI KITAIFA

# Kero vibali mazingira NEMC yapata ufumbuzi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KILIO cha upatikanaji vyeti vya tathmini ya mazingira (EIA) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali kimepatiwa ufumbuzi na sasa vitatolewa ndani ya siku 14 hadi 30 badala ya siku 105 za awali.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), katika ripoti yake ya mwaka 2019/20, pia aliwahi kusema jambo hilo linalotekelezwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), linachukua muda mrefu kukamilika, wastani wa siku 95, hivyo kukwamisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Ufumbuzi wa kero hiyo ambayo imekuwa ikilalamikiwa na makandarasi wanaotekeleza miradi mbalimbali, umefikiwa baada ya kikao cha Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Andrea Kundo na Naibu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Hamad Hassan Chande. Naibu mawaziri hao walikutana kujadili suala hilo ili kupata ufumbuzi wa kero ya ucheleweshwaji wa vibali vinavyotolewa na NEMC.

Katika kikao hicho kilichofanyika katika ukumbi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) jijini Dodoma jana, ilibainishwa kuwa kuchelewa kwa upatikanaji wa vibali hivyo, kumekuwa kikwazo katika miradi ya mawasiliano iliyokuwa ikihitaji vibali kutoka NEMC.

Naibu Waziri Kundo na Naibu Waziri Chande katika nyakati tofauti, waliagiza wataalamu wa wizara hizo mbili kukaa na kuunganisha mifumo yao, ili kusomana na kuondoa visingizio vya kutopatikana vibali kwa wakati.

Kundo alisema dosari hiyo ilisababisha kuchelewa kukamilika kwa miradi ya serikali kwa zaidi ya miezi saba, jambo ambalo lilikuwa likirudisha nyuma utendaji na ufanisi wa kazi za serikali kwa wakati.

Alisema sasa vibali vitaanza kutoka ndani ya siku 14 mpaka 30 kutoka siku 105 za awali, ambazo zilikuwa kikwazo kwa makandarasi waliokuwa wanatekeleza miradi mbalimbali, ikiwamo minara ya mawasiliano.

Naye Naibu Waziri Chande alisema kikao kazi hicho kimezaa matunda ambayo ni manufaa kwa taifa na vizazi vijavyo kwa kuwa kimekuwa na maridhiano makubwa na muhimu.

Alisema pamoja na makubaliano hayo yatakayosababisha maendeleo ya uwekezaji, lazima wananchi kuzingatia umuhimu wa utunzaji wa mazingira kwa sababu bila mazingira hakuna maisha.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, ameahidi kufanya kazi na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), ili kuweka mazingira mazuri ya kufanya kazi hizo.

Alisema atatekeleza maelekezo yaliyotolewa na naibu mawaziri hao ikiwamo kutoa vibali kwa wakati kama ilivyotakiwa kutolewa ndani ya siku 14 mpaka 30.



Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali Benjamin Mkapa, Dk. Alphonce Chandika (katikati), akipata maelezo kutoka kwa Mhariri wa Nipashe Wikiendi, Epson Luhwago (kulia), alipotembelea chumba cha habari cha kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Mikocheni, mkoani Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa TGL, Joyce Luhanga. **PICHA: JOHN BADI**

# Donge nono la mil. 10/- unapata ukimwona rubani, ndege iliyopotea

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

RUBANI wa ndege 5H -WXO inayomilikiwa na Shirika la PAMS, Samwel Gibuyi, ameripotiwa kupotea na ndege ya shirika hilo.

PAMS ni shirika la uhifadhi wa wanyama katika hifadhi ya jumuiya ya Nalika iliyoko Kijiji cha Matemanga, wilayani Tunduru.

Taarifa iliyotolewa jana na shirika hilo ilibainisha kuwa rubani huyo alipotea akiwa na ndege ndogo ambayo hutumiwa na shirika hilo kwa ajili ya doria na kufukuza wanyama wakali wanapoyakaribia makazi ya wananchi.

Meneja Mradi wa Shirika hilo Ukanda wa Kusini, Oscer Bubambezi, alidai kuwa rubani huyo aliruka na ndege hiyo Oktoba 18, mwaka huu katika Kituo cha Kiuma wilayani Tunduru majira ya saa 09:09 alasiri akiwa katika Hifadhi ya Pori la Akiba Selous Kingupira wilayani Rufiji mkoani Pwani.

Bubambezi aliendelea kubainisha kuwa kwa bahati mbaya Rubani Gibuyi hakufika katika kituo alichokuwa amekusudia kwenda na hajarudi hadi jana alipokuwa anatoa taarifa.

Alisema kuwa hali hiyo imewatia wasiwasi na kuwafanya waripoti katika Mamlaka ya Anga Tanzania ili wasaidiwe kufanya doria za ardhini na angani kumtafuta katika pori hilo.

Alisema kwa kuwa wameshindwa kupata mafanikio katika doria zao za awali, shirika limeahidi kutoa Sh. milioni 10 kwa mtu yeyote atakayetoa taarifa zitakazosaidia kupatikana kwa rubani wao.

Ofisa Wanyamapori wa Wilaya ya Tunduru, Limbega Hasan, alikiri kuwapo kwa tukio hilo na kubainisha kuwa serikali inatoa ushirikiano wa hali na mali katika kumtafuta rubani huyo.

Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, pia alithibitisha kuwapo kwa tukio hilo na kwamba juhudi za kuitafuta ndege hiyo pamoja na rubani wake zinaendelea kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kupitia ndege tano zinazopita angani, magari, pikipiki na watu wanaotembea kwa miguu katika pori hilo.

# Korti yampoka mirathi mke wa Bilionea Msuya

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Arusha imempoka Miriam Mrita, mjane wa aliyekuwa mfanyabiashara tajiri wa madini ya tanzanite, Bilionea Erasto Msuya, usimamizi wa mirathi ya mumewe.

Chini ya Jaji Devota Kamzola, mahakama hiyo juzi ilitengua haki hiyo ya usimamizi wa mirathi ya Bilionea Msuya baada ya mke wa marehemu kudaiwa kushindwa kugawa mali za marehemu kwa wakati.

Msuya aliuawa kwa kupigwa risasi 22, Agosti 7, 2013, majira ya saa 6:30 mchana katika eneo la Mijohoroni, kando ya barabara kuu ya Arusha-Moshi, karibu na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA).

Jaji Kamzola alisema kuwa mahakama hiyo, baada ya kupitia hoja za pande zote mbili imejiridhisha pasipo shaka kwamba mali za marehemu hazikuwahi kukusanywa, kutolewa taarifa na kugawanywa kwa wanufaika katika kipindi cha miaka tisa tangu msimamizi wa mirathi ateuliwe.

Mahakama hiyo imewapa baraka watoto wawili wa Bilionea Msuya, Glory Msuya na Simon Kelvin Msuya kuwa wasimamizi wa mirathi.

Vilevile, Jaji Kamzola aliagiza katika kipindi kisichozidi miezi sita wasimamizi wa mirathi hiyo wawe wamekusanya, kuhakiki madeni, kugawanya mali kwa wanufaika na kutoa taarifa mahakamani.Shauri hilo Na. 66 la mwaka 2019 la kumpinga msimamizi wa mirathi, lilifunguliwa na Ndeshukurwa Msuya, ambaye ni mama wa marehemu Bilionea Msuya dhidi ya mkwe wake, Miriamu Mrita.

Mjane huyo aliteuliwa na mahakama Novemba mwaka 2013, kuwa msimamizi wa mirathi kupitia shauri la mirathi Na. 8 la mwaka 2013.

Ndeshukurwa kupitia mawakili wake, Ismail Sharua na Fadhili Nangawe, waliomba mahakama hiyo imtengue Miriamu Mrita kuwa usimamizi wa mirathi ya mwanawe kwa madai kwamba tangu ateuliwe hakuwahi kukusanya, kufunga na kugawanya mali kwa wakati.

Hoja nyingine zilizowasilishwa na mawakili hao ni kwamba Miriamu Mrita anakabiliwa na kesi ya mauaji.

Pia alidaiwa kushindwa kumjali kwa matumizi mtoto wa marehemu mumewe, Glory Msuya, aliyekuwa nje ya nchi, kwa kumpatia fedha za ada, nauli ya kurejea nchini pamoja na matumizi binafsi.

Wakati hukumu hiyo ikisomwa na Jaji Kamzola, mjibu maombi, Miriam Mrita, alikuwa akiona na kusikilizwa kupitia mtandao wa mahakama, akiwa katika Gereza la Segerea jijini Dar es Salaamu.

**NJE YA MAHAKAMA**

Akizunguma baada ya kutolewa uamuzi huo, Ndeshukurwa Msuya, aliishukuru mahakama hiyo kwa kutenda haki, akiamini watoto wa marehemu watakuwa na haki ya kusimamia na kunufaika na mali za baba yao na sio mtu mwingie yeyote.

"Mimi sikuhitaji mali yoyote ya mwanangu, nilichotaka ni mali zote zisimamiwe na watoto na sio mtu mwingine yeyote. Kama familia tumepokea kwa furaha uamuzi mahakama na haki imetendeka," alisifu.

Akizungumza kwa Miriam Mrita, Steven Mrita, ambaye alikuwa msimamizi wa mali za marehemu, alisema wameridhika na uamuzi wa mahakama na hawatakuwa na pingamizi lolote.

# TAMWA yalaani rushwa ya ngono vyuo vikuu

**Na Enock Charles**

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) kimelaani tukio la Mhadhiri Petrol Mswahili wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kudaiwa kujihusisha na kimapenzi na wanafunzi wa kike chuoni huko katika mazingira yanayotajwa kuwa ya rushwa.

Katika taarifa iliyotolewa na TAMWA jana ikinukuu taarifa ya chuo hicho kuhusiana na tukio la mhadhiri huyo, Mkurugenzi wake, Rose Reuben, alisema wamesikitishwa na tukio hilo linaloashiria uwapo wa rushwa ya ngono, jambo ambalo ni kinyume cha maadili ya utumishi wa umma.

"TAMWA ikiwa ni taasisi inayopinga unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake ikiwamo rushwa ya ngono, tunalaani tukio hilo linalovunja maadili ya utumishi wa umma na zaidi hasa kudhalilisha watoto wa kike katika taasisi hii ya elimu ya juu.

"Mwaka 2019 TAMWA ilifanya tathmini ya kuangazia ukubwa wa rushwa ya ngono kwenye vyumba vya habari, maeneo ya kazini na taasisi za elimu ya juu na kubaini kuwa tatizo hilo lipo kwa ukubwa wake," TAMWA ilisema katika taarifa yake hiyo.

Chama hicho kimeupongeza uongozi wa UDOM kwa kuchukua hatua za haraka dhidi ya mhadhiri huyo, kikishauri uongozi wa chuo kuweka mikakati itakayokomesha vitendo hivyo na kwamba uchunguzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) utakapokamilika, sheria ichukue mkondo wake.

"Tunaiomba TAKUKURU iendelee kushirikiana na wadau kutoa elimu kuhusu rushwa ya ngono na udhalilishaji mwingine wa kijinsia," TAMWA inashauri katika taarifa yake hiyo.

Mwaka 2019, Nipashe ilichapisha ripoti kwa siku tatu mfululizo ikiangazia namna rushwa ya ngono inavyofanyika vyuo vikuu nchini, ikihusisha: Mhadhiri kwa mwanafunzi; mhadhiri kwa mhadhiri; mwanafunzi kwa mwanafunzi; na mhadhiri au ofisa utawala chuoni na mfanyakazi (wa ngazi ya chini) chuoni.

# 5,000 wapangiwa mikopo ya HESLB awamu ya IV

**Na Halfani Chusi**

BODI ya Mikoo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HELBS) imetangaza kutoa nafasi kwa wanafunzi ambao hawajaridhika na viwango vya mikopo, kuwasilisha maombi ya kuongezewa.

Imesema dirisha hilo la rufani limepangwa kufunguliwa Novemba 6 na matokeo ya rufani hizo yatatangazwa kabla ya Novemba 20 mwaka huu.

Jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji Bodi hiyo Abdul-Lazaq Badru, alitangaza nafasi hiyo alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu orodha ya nne yenye wanafunzi wapya 5,003 wa mwaka wa kwanza waliopangiwa mkopo wenye thamani Sh. billion 11.6.

Alisema jumla ya wanaufaika wa mwaka wa kwanza sasa imefikia 65,339 ambao wamepangiwa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 169.8.

"Orodha hii ya nne ina wanufaika 5,003 ambao muda wowote kuanzia sasa (jana alasiri) wanaweza kuingia katika akaunti zao za SIPA walizoombea mikopo na kupata taarifa zaidi," alisema.

Badru alibainisha mchanganuo wa wanufaika hao 65,359, akisema kuwa 1,133 ni yatima waliofiwa na wazazi wote wawili, 9, 450 waliofiwa na mzazi mmoja, 198 ni wanafunzi wenye ulemavu, 2,919 waliofadhiliwa na taasisi mbalimbali katika masomo ya sekondari na 51,559 wanatoka kwenye kaya maskini.

"Takwimu hizi mtaona kuwa ile dhamira ya serikali kuwawezesha vijana kutoka katika kaya maskini inathibitika ambapo wote mnaona. Asilimia 41 ya wanufaika 65,359 ni wanawake na asilimia 59 ni wanaume," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema bodi hiyo bado inakamilisha malipo ya wanafunzi 74,440 ambao ni wanufaika wanaoendelea na masomo baada ya kupokea matokeo ya mitihani yanayothibitisha kuwa wamefaulu kuendelea na masomo.

"Tuna wanufaika 98,000 wanaoendelea na masomo na hadi leo (jana) Ijumaa Oktoba 29, tumepokea matokeo ya mitihani ya wanafunzi 74,440 waliofaulu na tutaanza kutuma fedha kesho (leo)," alisema.

Mwenyekiti Jumuiya ya Wanafunzi Taasisi za Elimu ya Juu, Frank Nkinda, aliishukuru serikali kwa kutoa mikopo hiyo na kuiomba kuendelea kusaidia wanafunzi wengi kupata fursa ya kusoma elimu ya juu.



Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, mkoani Ruvuma, Julius Mtatiro, akizungumza na wakulima waliojitokeza kwenye mnada wa kwanza wa zao la korosho, katika Kijiji cha Namakambale, Tarafa ya Nakapanya, wilayani humo jana. **PICHA: STEVIE CHINDIYE TUNDURU**

# Tanzania yaishukuru WB utekelezaji miradi

**Na Benny Mwaipaja**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, ameishukuru Benki ya Dunia kwa kuwekeza zaidi ya dola za Kimarekani bilioni 5.5 (takriban Sh. trilioni 12.6) kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo nchini.

Dk. Nchemba alitoa pongezi hizo jana wakati akizungumza na Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia, Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika, Dk. Hafez Ghanem, wakati wa Mikutano ya Mwaka ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), iliyofanyika kwa njia ya mtandao, jijini Dar es Salaam.

"Miongoni mwa fedha hizo ni pamoja na Dola bilioni 1.167 zilizotolewa na benki hiyo kwa ajili ya kutekeleza miradi mitano ya maendeleo ikiwamo ya elimu, miundombinu, umeme na Tanzania ya Kidijitali kwa lengo la kuchochea uchumi jumuishi na kupambana na umasikini," alisema.

Dk. Nchemba alisema kiasi hicho cha fedha kinahusisha utekelezaji wa miradi 26 ya maendeleo inayopata fedha kupitia dirisha la mikopo nafuu (IDA) la Benki ya Dunia yenye thamani ya Dola bilioni 5.502. Alisema miradi 21 kati ya hiyo ni ya kitaifa yenye thamani ya Dola bilioni 4.804 na miradi mitano ni ya Kikanda yenye thamani ya Dola bilioni 0.698 na kwamba mpaka sasa Dola bilioni 1.932 zimetolewa sawa na asilimia 35 ya fedha zote. Kuhusu hatua zinazochukuliwa kupambana na athari za kiuchumi na kijamii zilizosababishwa na corona, Dk. Nchemba alisema serikali imeandaa mpango wa mwaka mmoja wa kukabiliana na athari hizo utakaogharimu Sh. trilioni 3.62.

"Tayari serikali imepokea Dola milioni 567.25 (takriban Sh. trilioni 1.3) kutoka IMF zikiwa ni mkopo nafuu kwa ajili ya kunusuru maisha ya watu na uchumi wa nchi kutokana na athari za corona," alisema.

Fedha hizo, alisema zimeelekezwa kutatua changamoto mbalimbali kwenye sekta za utalii, kunusuru kaya masikini, maji, elimu na afya upande wa Tanzania Bara na Zanzibar, hivyo akatoa wito kwa wadau wengine wa maendeleo kuunga mkono jitihada hizo ili kusisimua uchumi wa nchi.

Pia alisema hivi karibuni serikali inatarajia kukamilisha mazungumzo na Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata fedha za miradi miwili ukiwemo wa kuboresha masuala ya ardhi na kuongeza msukumo wa kujifunza kupitia elimu ya msingi.

Kuhusu wanafunzi wanaoacha masomo, Dk. Nchemba alimwambia Dk. Hafez kwamba changamoto ni kubwa na takwimu zinaonyesha kuwa wanafunzi (wasichana na wavulana) 198,620 waliacha masomo katika shule za msingi wakati wanafunzi kwa sekondari ni 113,484 kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo vifo, utoro, utovu wa nidhamu na ujauzito.

Dk. Hafez aliipongeza Tanzania kwa hatua mbalimbali inazozichukua katika kusimamia uchumi na maendeleo ya wananchi wake.

Aliahidi kuwa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya Dunia itakutana hivi karibuni kujadili maombi mbalimbali ya fedha yaliyotolewa na Tanzania kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ili fedha hizo zipatikane kwa wakati.

HABARI KITAIFA

# Kunenge atoa neno kuhusu fedha NGO

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakari Kunenge ameyaelekeza mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) yanayofanya kazi zake katika mkoa huo kutumia fedha wanazoomba kwa wafadhili kuwasaidia wananchi badala ya kujinufaisha wenyewe.

Kunenge alitoa maelekezo hayo wakati wa kikao kazi na mashirika yasiyo ya kiserikali kilichofanyika jana mjini hapa.

Alisema hategemei kusikia kuna NGO za mfukoni na za kifamilia ambazo zinawanufaisha watu wachache badala ya walengwa ambao ni wananchi.

Kunenge alizitaka NGO hizo kuwa wazi kuirahisishia serikali kutambua ni huduma gani inatolewa na itakuwa kwa muda gani pamoja na manufaa yake kwenye jamii badala ya kufanya kazi bila taarifa kwa serikali na jamii inayonufaika.

Kunenge alisema serikali ina wajibu wa kutoa huduma kwa wananchi, lakini kuna masuala ambayo peke yake haiwezi kufanya na uwapo wa mashirika hayo unasaidia kutekeleza baadhi ya mahitaji.

"Mwananchi ana mahitaji mengi na hapo ndipo tunapoona umuhimu wa mashirika binafsi, ni vyema tuzingatie malengo ya kuanzishwa kwa mashirika," alisema.

Mjumbe wa Baraza la Taifa la Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Gaidon Haule, alisema mkoa huo una mashirika 390 na kati ya hayo 133 pekee yamehakikiwa.

Alisema mashirika hayo yanakabiliwa na vikwazo mbalimbali vikiwamo vya kukosekana kwa mwendelezo baada ya fedha za wafadhili kuisha pamoja na uwapo wa sheria, kanuni na taratibu kandamizi katika utekelezaji wa shughuli za NGO.

Kikwazo kingine kilichoelezwa ni baadhi ya mashirika kutofuata sheria na taratibu ikiwamo uwasilishwaji wa taarifa za utekelezaji wa shughuli zao na za mapato ya matumizi na mapato ya fedha kutoka kwa wafadhili.

Katika taarifa yake alibainisha mapendekezo kwa serikali kuimarisha ushirikiano na mahusiano ya kazi baina yake na mashirika hayo.



Mkuu wa Wilaya ya Kipolisi Msalala, SSP Thomas Kiondo akizungumza na askari wa jadi maarufu kama Sungusungu 300 kutoka vijiji sita vya Kata ya Segese, Halmashauri ya Msalala, wakati wa ufungaji wa mafunzo ya ulinzi na ukamataji salama kwa ajili ya kupambana na uharifu wa uporaji mifugo na madini kwenye maneo yao, mapema wiki hii. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Waonywa kupanda magari ya wenye kesi

**Na Munir Shemweta,** MOROGORO

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewataka wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kujiepusha kutumia usafiri wa wananchi wanaoshitakiana wakati wa kwenda uwandani.

Amesema hatua hiyo itawaepusha dhidi ya tuhuma za kufanya upendeleo wakati wa kusikiliza mashauri.

Dk. Mabula alitoa kauli juzi mjini hapa wakati akishuhudia uapishwaji wajumbe wapya wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro uliofanywa na Mkuu wa Mkoa huo, Martine Shigela. Baraza hilo linahudumia halmashauri wilaya za Mvomero na Morogoro pamoja na Manispaa ya Morogoro.

"Ninaomba hili mliepuke sana maana linaleta changamoto kubwa na mwingine anaweza akakata rufani akidai mwenzake alikuwa anawapeleka wajumbe uwandani. Suala hilo limekuwa likileta shida sana," alisema Dk. Mabula.

Alisema wajumbe wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya wana jukumu la kusikiliza kesi na kutoa maoni juu ya shauri husika kwa maandishi na wakati wa kusikiliza shauri, hivyo wana wajibu wa kuhoji maswali ya ufafanuzi ili kupata uelewa zaidi.

Maoni ya wajumbe, alisema yanatumika kumsaidia Mwenyekiti wa Baraza kutoa uamuzi ingawa ni lazima mwenyekiti ajikite katika sharia, hivyo anaweza kuyakubali maoni hayo au kuyakataa lakini lazima atoe sababu za kuyakataa.

Dk. Mabula alisema, wizara inachoshauri ni Mwenyekiti wa Baraza awe na ratiba ya mwezi mzima kuhusiana na safari za kwenda uwandani na taarifa iwasilishwe kwa Mkuu wa Wilaya pamoja na Mkurugenzi wa Halmashauri husika ili inapofika siku ya kwenda uwandani, watumie usafiri wa serikali.

Aliongeza kuwa kutumia usafiri wa serikali kutaepusha minong'ono na kumkosesha amani mmoja wa wanaoshitakiana kwa kuhisi kuwa anaweza kuwa anaonewa.

Aidha, Naibu Waziri alitaka mashauri katika mabaraza ya ardhi kumalizika katika kipindi kisichozidi miezi sita labda kwa yale ambayo yanaweza kucheleweshwa kwa sababu za mawakili.

Mkuu wa Mkoa, Martine Shigela, aliwapongeza wajumbe wa baraza walioteuliwa na kuwaeleza kuwa uteuzi walioupata umezingatia uadilifu na weledi wao na ana matumaini watatenda haki kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa.

Wajumbe wanne wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro waliapishwa kuhudumu kwenye baraza hilo na sababu ya mabaraza ya ardhi na nyumba kuketi na wajumbe katika kusikiliza mashauri ni kushirikisha jamii kwenye utatuzi wa migogoro ya ardhi.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro, Mwanahawa Kassim, hadi Septemba, mwaka huu, kulikuwa na mashauri 1,220 na kati ya hayo yaliyofunguliwa kwa Septemba pekee ni 57 na yaliyoisha mwezi huo ni 114.

# Madiwani wacharuka bei juu mbolea

**Na Thobias Mwanakatwe,** SONGWE

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya Mbozi mkoani hapa wameeleza kushangazwa na kupanda kwa bei ya mbolea maradufu ambayo sasa imefikia Sh. 100,000 hadi 120,000 kwa mfuko mmoja huku bei ya bia ikishuka, kuleta taharuki kwa wakulima.

Wamesema inashangaza mbolea aina ya DAP kupanda kwa kiasi hicho, hivyo kuiomba serikali itoe tamko kuhusu hali hiyo.

Madiwani hao walihoji suala hilo jana kwenye kikao cha Baraza la Madiwani kwamba hali hiyo inahatarisha kushuka kwa uzalishali wa mahindi katika msimu wa kilimo wa mwaka huu.

Diwani wa Viti Maalum, Mesiah Swela, ndiye aliyeibua suala hilo kwa kuomba mwongozo kwenye kikao hicho na kuhoji inakuweje mbolea yenye ujazo sawa hapa nchini iuzwe kwa 120,000, lakini nchi jirani za Zambia na Malawi inauzwa kwa Sh.70,000. Swela ambaye aliungwa mkono na madiwani wenzake, alisema hoja ya kwamba bei ya mbolea imepanda kutokana na janga la corona haina mashiko kwa sababu nchi jirani nazo zilikumbwa na janga hilo lakini bei haijapanda kama ilivyo nchini. Diwani wa Itaka, Allan Mgula, aliunga hoja hiyo akisema ni wakati mwafaka wa serikali kujitokeza na kutoa tamko juu ya kupanda kwa bei ya mbolea kwa kuwa hatua hiyo inahatarisha hali ya uzalishaji wa chakula nchini.

Ofisa Tarafa ya Vwawa, Haji Ibrahim, aliyemwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Mbozi, Cosmas Nshenye, alisema ni vizuri viongozi wakawa watulivu kwa kuwa suala hilo limefikishwa serikalini.

" Waheshimiwa madiwani najua mnapata shida sana mnapoenda kwenye mikutano kwani ni lazima muulizwe kuhusu kupanda kwa bei ya mbolea. Niwaombe muwe wavumilivu na tuendelee kulisukuma suala hilo ili serikali ifanyie kazi," alisema Ibrahim.

"Wote tunatambua kuwa tangu suala la corona liibuke, nchi nyingi zilijifungia na viwanda vingi vilisimamisha uzalishaji,' aliongeza.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Nidhamu mbovu Ligi Kuu Bara 'mfupa' unaokomaa*

**LIGI** Kuu ya NBC Tanzania Bara ndio ligi ya juu hapa nchini na msimu huu mwaka 2021/22 inashirikisha jumla ya timu 16 kutoka mikoa mbalimbali.

Timu hizo zinazoshiriki ni mabingwa watetezi, Simba, Yanga, Azam, Mtibwa Sugar, Kagera Sugar, Ruvu Shooting, Polisi Tanzania, Dodoma Jiji, KMC, Biashara United, Geita Gold, Tanzania Prisons, Mbeya City, Mbeya Kwanza, Coastal Union na Namungo.

Mechi zote za ligi hiyo ambayo hutoa wawakilishi wa nchi katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho, inaonyeshwa mubashara kupitia Azam Media.

Kwa maana hiyo, mechi zote zinaonekana duniani kote kwa sababu kupitia simu za mkononi, wadau wa soka wanaweza kushuhudia mitanange mbalimbali inayochezwa hapa nchini.

Hata hivyo, wakati ligi hiyo ikiendelea kupanda viwango, bado kumekuwa na matukio mbalimbali ya aibu ambayo kila mara yanakemewa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), lakini yanajirudia na yamekuwa hayana afya katika maendeleo la soka nchini.

Viongozi wa timu, makocha au wanachama wanaojulikana kwa jina maarufu la 'makomandoo' wamekuwa wakionekana kwenye picha mnato au za video wakiongoza wachezaji kupitia milango isiyo rasmi kwa madai ya kukwepa ushirikina.

Wakati mwingine timu hizo zikiwa zinawasili viwanjani na wakifahamu wazi kamera ziko mbele yao, viongozi hao wanawaongoza wachezaji kufanya vitendo vinavyotafsiriwa au vinavyohusishwa moja kwa moja na imani za kishirikiana.

Tumeshuhudia pia wakati mwingine viongozi hao wakiwakataza wachezaji kutoingia kwenye vyumba rasmi za kubadilishia nguo wakidai vimepulizwa dawa za kuwalegeza nyota wao ili washindwe kucheza kwa viwango vya juu na kutumia magari waliyokuja nayo au kukaa chini ya miti.

Haya yanayoendelea hayaendani na maandalizi makubwa yaliyofanywa na viongozi husika kuanzia kwenye mchakato wa usajili, kambi za ndani na nje ya nchi, michezo mbalimbali ya kirafiki waliyocheza, kuendelea kufanya 'mauzauza' haya kunashusha heshima ya ligi. Wakati wadau wengine wakiitaka TFF kuongeza kiwango cha faini kwa timu zinazorudia makosa hao mara kwa mara, umefika wakati kanuni kali zikawekwa ili kuitokomeza tabia hii 'mbovu' inayoonekana kukomaa au kuonekana kama ni jambo la kawaida.

Kutokana na teknolojia na vyombo vya dijitali vinavyotumika, si wakati wa kuendelea kufanya vitendo hivi kwa sababu mbali na kuivunjia heshima ligi, lakini havitoi taswira yenye afya kwa wachezaji chipukizi ambao baadaye wanatarajiwa kuitumikia nchi.


Si tu matukio haya yanashusha heshima ya ligi, lakini pia yanapunguza hadhi ya klabu, wachezaji na wote wanaoshiriki. Na kwa sababu baadhi humulikwa na kamera, basi hujipunguzia heshima au dhamana waliyopewa na wanachama wao kwa kuweka mbele imani za kishirikina hali ya kuwa waliwaaminisha wamefanya usajili mzuri na maandalizi sahihi kuelekea msimu husika.

Adhabu za faini ambazo zimekuwa zikitolewa kwa wahusina zinaonekana kulipika hivyo, hivyo wahusika wanaendelea kurudia makosa hayo mara kwa mara.

Tuachane na vitendo hivyo kwa maslahi ya soka letu, haipendezi kuipa Kamati ya Mashindano ya TFF kazi ya kutunga kanuni kali na badala yake wahusika wakaacha tabia hizo, wasijifishe kwenye 'kivuli' cha kufanya ushirikina ili kuhalalisha kupatiwa fedha za kukamilisha mchakato huo.

Tunawakumbusha wale wote wanaosimamia timu kuacha mara moja kufanya matukio haya kwa sababu tunahitaji kuona Tanzania inasifika kwa mambo mazuri, na kila mmoja afahamu mpira wa miguu ni mchezo unaohitaji maandalizi bora na matokeo chanya kamwe hayapatikani na njia za miujiza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# *Hasama ndimi za moto*

Na Barnabas Maro

**"HASAMA"** ni uadui. Makala hii yaeleza uadui au adawa ni kama ndimi za moto ambazo huchoma. Methali hii inatuhimiza tujiepushe na uadui ambao unaweza kutuletea maangamizo.

Pia husemwa "Hasara humfika mwenye mabezo". Mabezo ni dharau au mapuuza yanayotokana na dharau dharau. Aghalabu hasara humpata mtu mwenye tabia ya kupuuza mashauri apewayo. Methali hii yatukanya tusiwe na tabia ya kupuuza mashauri tunayopewa tusije tukafikwa na hasara.

Mchezo ni jambo linalofanywa kwa nia ya kuburudisha. Jambo ambalo watu au timu hufanya kwa kushindana ili kupata mshindi. Mchezo wa mpira wa miguu kwa mfano, unapendwa sana kwani huvuta watazamaji wengi kuliko michezo mingine.

Pia ni kazi ya sanaa ambayo huigizwa kwa ajili ya kuelimisha na kuburudisha watu.

Maana moja ya neno 'shonde' ni hali ya watu kuto- semezana kutokana na ugomvi wao wa zamani; mfundo, chuki, uhasidi. Simba na Yanga zamani zilikuwa timu moja lakini tangu zilipotengana zimekuwa mahasimu yaani watu wanaochukiana; maadui! Kwanini wawe hivyo ilhali (pamoja na kuwa) ni timu za jiji moja?

Husemwa: "Asiyeona aibu zake asione za mwenziwe." Ikiwa mtu hawezi kuona udhaifu wake mwenyewe asilalamikie watu wengine. Methali hii huweza kutumiwa kwa mtu ambaye anapenda kuwashutumu na kuwalaumu watu wengine au kuziona dosari zao ilhali ana dosari sawa na wao!

> **Husemwa: "Asiyeona aibu zake asione za mwenziwe." Ikiwa mtu hawezi kuuona udhaifu wake mwenyewe asilalamikie watu wengine. Methali hii huweza kutumiwa kwa mtu ambaye anapenda kuwashutumu na kuwalaumu watu wengine au kuziona dosari zao ilhali ana dosari sawa na wao!**

Kinachowaumiza Simba na Yanga ni chuki zao, hasa zinazosababishwa kwa kiasi kikubwa na mashabiki wao wasiojua katika mchezo wowote kuna kushinda, kushindwa na sare.

Baadhi ya wanachama wao wasio na fikra yaani mawazo yaliyomo kichwani mwa kiumbe dhana, hufuata mkumbo bila kujua athari zake!

Mara nyingi shabiki ni mtu asiye na msimamo kwani ajuacho ni ushindi tu. Watu wa aina hii hawataki kusikia neno "shindwa" ila "shinda" tu. Ndio maana huwa rahisi kwao kuzikimbia timu zao zinaposhindwa na kwenda kushabikia timu iliyoshinda tu!

Hayo ndiyo wanaozizomea timu walizozikimbia na huwa hodari kuzishangilia timu ngeni kutoka nje ya Tanzania zinaposhindwa timu zao walizozikimbia!

Wahenga walisema; "Afiriti hafichiki." Afiriti ni mtu mwovu au mwenye matendo maovu. Maana yake mtu mbaya hafichiki. Methali hii hutumika kutukumbusha uovu na matendo mabaya hayawezi kufichika, kwani lazima kunasiku yatajitokeza. Mathali hii huweza kutumiwa kumgundua mtu mwovu.

"Akili ya mtu ndiyo wazimu wake." Maana yake akili ya mtu yaweza kuwa wazimu wake pia. Hutumiwa kuelezea kuwa akili ya binadamu yaweza kuzua mema na mabaya pia. Ndo maana baadhi yetu huzishangilia timu ngeni kwa vifiji (hoihoi) zinapokuja kucheza hasa na timu za Simba na Yanga kumbe twajidharaulisha wenyewe!

Ebo! (tamko linaloonyesha hisia ya dharau inayotokana na kukasirika au kutoridhika.) Pukachaka! (neno lenye kuashiria kutema mate ambalo humaanisha kukidharau kitu kilichotajwa.)

"Fedheha za mwenzio uzifurahie." Sio tabia njema kufurahia aibu au fedheha zilizomfika wenzio. Hutufunza umuhimu wa kutowacheka wenzetu wanapopatwa na matatizo kwani sisi pia tunaweza kupatwa na matatizo hayo. Leo ni kwao kesho ni kwetu.

Aidha, " Chako chako peke yako, kikikufika kina wenzako." Maana yake kilicho chako ni chako pekee lakini kinachokupata huwapata wenzako. Tunasihiwa kwamba lazima tuingiliane na watu wengine kwa kuwa binadamu huweza kujifaa katika kila jambo. Yafaa kusikiliza ushauri au waadhi tupewao na wenzetu.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784335096**

HABARI KITAIFA

# Wafugaji waamuriwa kuondoka shamba la mpunga

**Na Julieth Mkireri,** RUVU

OFISA Tarafa ya Chalinze, Thomas Molel, ameagiza wafugaji wanaolisha mifugo yao karibu na mashamba ya wakulima wa mpunga Ruvu, kuondoka mara moja na kuonya hatua kali zitachukuliwa kwa watakaokaidi.

Mollel alitoa agizo hilo jana wakati wa ufunguzi wa wiki ya Chama cha Ushirika wa Wakulima wa Umwagiliaji Ruvu (CHAURU) uliofanyika katika makao makuu ya ushirika, Kijiji cha Visezi Kata ya Ruvu.

Moleli ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Aboubakar Kunenge, katika hafla hiyo, alisema kuna mifugo inalishwa kwenye mashamba ya mpunga Ruvu na kusababisha uharibifu wa miundombinu ya mifereji ya shamba hilo.

"Wafugaji watafute mahali pengine pa kulisha mifugo yao. Hapa si sehemu sahihi kwao na yeyote atakayekamatwa sheria itachukua mkondo wake. Katika hili hakuna uvumilivu tena nendeni maeneo mliyotengewa," alisema.

Mollel alitoa agizo hilo, baada ya kundi la wafugaji kuwapiga na kuwajeruhi baadhi ya wakulima wa mpunga katika shamba la CHAURU, akiwamo Mwenyekiti wa Ushirika huo, Sadala Chacha.

Awali, akitoa taarifa ya ushirika huo, Meneja wa CHAURU, Victoria Olotu, alisema uwekezaji wa kilimo cha mpunga katika eneo lenye miundombinu ya umwagiliaji umeongezeka kutoka hekta 334 hadi 720.

Olotu alisema katika uzalishaji wa mpunga, tija imeongezeka kutoka tani 3,000 mwaka 2017 hadi tani 5,000 mwaka 2020. Pia baada ya kuhamasishwa kuhusiana na kilimo cha korosho, tayari wamelima ekari 200, ambazo zimeanza kutoa matunda.

Kuhusu vikwazo wanavyokabiliana navyo, alisema ubovu wa miundombinu umesababisha kuongezeka kwa gharama za uzalishaji kwa sababu maji ya umwagiliaji hayafiki kwa wakati na kwa wingi uliokusudiwa, hivyo kupunguza uzalishaji kwa asilimia 40.

Meneja huyo alieleza vikwazo vingine wanavyokumbana navyo kuwa ni mifugo kulishwa ndani ya mashamba ya mpunga hali ambayo imepunguza ubora wa mashamba na kuyafanya kuwa na miinuko.

Octoba 25, mwaka huu, Mwenyekiti wa CHAURU akiwa na baadhi ya wanachama katika shamba la ushirika huo, walikutana na zaidi ya watu 20 jamii ya wafugaji, ambao waliwavamia na kuwapiga kwa fimbo na kuwasababishia majeraha.

Katika purukushani hizo, mgambo na baadhi ya wanachama walikimbia na kuwaacha Chacha kupigwa na kujeruhiwa kichwani na mkononi huku mwenzake Daniel Mwita akijeruhiwa mkononi.

Kutokana na vurugu hizo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema baada ya kufanyika msako, watu wawili jamii ya wafugaji walitiwa mbaroni wakituhumiwa kuhusika katika tukio hilo.

## RC aonya matumizi fedha za mkopo

**Na Gurian Adolf,** KALAMBO

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Joseph Mkirikiti ameziagiza halmashauri za mkoa huo fedha zilizotolewa kwa mkopo na wahisani kwa ajili ya kupambana na ugonjwa wa Uviko-19 zisitumike kukamilisha miradi viporo badala yake zitekeleze miradi mipya.

Agizo hilo alilitoa jana wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa Shule ya Wasichana Kambo na kusikitishwa baada ya kukuta Sh. milioni 60 zilizotolewa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa na fedha kumalizika bila kukamilisha ujenzi huo.

Alisema Serikali ya Mkoa wa Rukwa haitaki kuona fedha zilizotolewa na Rais Samia Suluh Hassan kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, zinatumika kukamilisha miradi ya zamani.

"Fedha hizi zilizotolewa na Rais ni kwa ajili ya kutekeleza miradi mipya katika sekta zilizokusudiwa na si kutumia kukamilisha miradi ya zamani, hivyo ni viporo vya halmashauri tafuteni fedha muikamilishe miradi hiyo," alisema.

Alisema wenye tabia ya kufanya ubadhirifu katika fedha za miradi ya maendeleo wajiandae kwa kuwa kamwe sheria haita waacha waendelee na mtindo huo.

Hata hivyo, aliwahimiza wananchi kushiriki katika kutekeleza miradi hiyo kwa kujitolea nguvu kazi ili rasilimali fedha iweze kutumika kutekeleza miradi mingine.



Mwanachama wa kikundi cha Nyusa, Kata ya Barikiwa, wilayani Liwale, mkoani Lindi, Hamza Ngabuja, akiweka mzinga wa nyuki juu ya mti baada ya kikundi hicho kupata mafunzo ya ufugaji bora wa nyuki juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wakumbushwa unyenyekevu, kujali wateja

**Na Joseph Mwendapole**

WATUMISHI wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), wametakiwa kuwatumikia wateja kwa unyenyekevu na kwa lugha ya staha, ili waone umuhimu wa kutumia usafiri wa haraka.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa DART, Dk. Eliphas Mollel, wakati akifungua mafunzo ya siku mbili kwa vijana wafanyakazi wa muda.

Vijana hao wamemaliza vyuo mbalimbali nchini na wanapewa mafunzo hayo, ili wakafanye kazi kwa muda kwenye mifumo ya DART kama sehemu ya mafunzo kwa vitendo, ili wapate uzoefu wa kuajiriwa sekta ya umma au binafsi.

Dk. Molle alisema vijana hao wanapaswa kuwa na lugha nzuri ya kuwavutia wateja, ili waweze kuona uzuri wa kutumia usafiri huo wa haraka na kuachana na matumizi ya daladala na magari binafsi kwenda kazini.

"Unapotoa huduma lazima utambue kuwa unawahudumia wananchi na sisi tunahudumia zaidi ya wananchi 150,000 kwa siku. Sasa ili kuwafanya wapende usafiri wetu lazima tuwe na lugha za kuvutia," alisema

Pia alisema huduma nzuri zitakazotolewa na watumishi hao, zitasababisha watu wanaotumia usafiri huo kuongezeka na iwapo hawatatoa huduma bora wanaweza kupungua.

Alisema vijana hao wanapaswa kutimiza wajibu wao wa kuhakikisha wale wanaotakiwa kupewa kipaumbele kama wazee na wajawazito wanahudumiwa kwa haraka na kwa ufanisi.

"Unapomuona mjamzito akiwa kwenye foleni, unatakiwa kumfuata na kumwambia kwamba hatakiwi kukaa kwenye foleni. Unamwelekeza sehemu ya kukaa au muda wa wanafunzi hakikisha wanapewa kipaumbele," alisema.

Dk. Mollel alisema kwa sasa wameainisha mabasi ya wanafunzi wakati wa kwenda shule na kurudi hivyo ni wajibu wa watumishi wa DART kufahamu hilo.

Alisema kujali wateja ni jambo muhimu kwenye biashara yoyote ile duniani, kwani kinyume na hilo wateja wengi watahamia kwa watu wenye lugha nzuri na wenye kujali wateja wao.

"Mfano nakuja kwenye duka lako wewe hujali unaendelea kuchati na simu mimi siwezi kuvumilia nitaondoka kwenda kwenye duka ambalo mhusika atanijali, sasa ukifanya hivyo mara nyingi unapoteza wateja wengi," alisema Dk. Mollel

Alisema usafiri wa haraka umesaidia sana watu kuwahi kazini na kwenye shughuli mbalimbali za kibiashara tofauti na ilivyokuwa kabla ya kuanza kwa usafiri huo.

"Zamani kutoka Kimara hadi Feri watu walitumia saa hata mbili, lakini kwa sasa kutoka huko Kimara hadi Feri unatumia dakika 35 tu, haya ni mapinduzi makubwa kwenye usafirishaji," alisema.

# Tanzania na USAID wateta kuinua kilimo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, amekutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), Kate Somvongsiri, katika Ofisi za Wizara ya Kilimo jijini Dodoma.

Katika mazungumzo hayo hayo, viongozi hao walijadili kwa kina kuhusu vipaumbele vya serikali katika Wizara ya Kilimo.

Pia walijadili umuhimu wa kutatua tatizo la kukosekana tija na uzalishaji mdogo kwenye mazao ya wakulima, ili kutafuta mwarobaini wa kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo nchini.

Viongozi hao pia walijadili umuhimu wa kuongeza nguvu na umuhimu katika sekta ya utafiti, ili kubaini nini kinahitajika katika ardhi ya kilimo kwenye maeneo mbalimbali ya wakulima nchini, ili wakulima watambue mazao yanayokubalika katika maeneo yao pamoja na kutambua aina na kiasi cha mbolea kinachohitajika.

Vilevile, majadiliano hayo yalijikita pia kwenye umuhimu wa kuboresha huduma za ugani, ambapo Waziri Mkenda alibainisha kuwa tayari wizara yake imeanza kuchukua hatua madhubuti ikiwa ni pamoja na kuwawezesha maofisa ugani kuwa na pikipiki ambazo zitawarahisishia kuwafikia wakulima kwa wakati.

Viongozi hao pia walijadili umuhimu wa Ugharamiaji wa Kilimo (Agro Financing), pamoja na kuwekeza kwenye Kilimo Anga.

Mkurugenzi Mkazi wa USAID, Kate Somvongsiri, alimweleza mwenyeji wake kuwa dhamira ya kushiriki katika kikao kazi hicho ni kujitambulisha kwake kujua vipaumbele vya wizara na kuandaa mkakati wa namna ya kushirikiana na serikali katika kutatua vikwazo vya kilimo.

# Mwongozo utoaji chakula elimumsingi wazinduliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imezindua mwongozo wa utoaji wa huduma ya chakula na lishe kwa wanafunzi wa elimumsingi, ili kuondokana na tatizo la utoro na kuongeza kiwango cha ufaulu.

Mwongozo huo umeandaliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali la Project Concern International (PCI) kwa ufadhili wa Serikali ya Marekani kupitia Idara ya Kilimo (USDA), ambao unalenga wazazi na wadau mbalimbali wa elimu kutambua umuhimu wa huduma hiyo.

Akizindua mwongozo huo jana jijini hapa, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Leonard Akwilapo, alisema takwimu za mwaka 2021 zinaonyesha kuna shule 23,835 za elimumsingi zenye wanafunzi 13,708,242, jambo linalochangia umuhimu wa utekelezaji wa mwongozo huo.

"Kuna uhusiano mkubwa sana kati ya afya ya mwanafunzi na maendeleo yake kitaaluma, kuna madhara makubwa kwa wanafunzi kukosa chakula shuleni, ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa usikivu wakati wa ujifunzaji, mahudhurio kuwa hafifu kusababisha utoro na wengine kukatisha masomo," alisema.

Mtendaji huyo wa wizara alisema hali hiyo pia husababisha kushuka kwa ufaulu wa wanafunzi katika majaribio ya mitihani yao.

"Upatikanaji wa chakula na lishe shuleni utaongeza hali ya wanafunzi kukaa shuleni na kuwa tayari kujifunza,"alisema.

Alifafanua kuwa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 inatamka wazi utoaji wa huduma muhimu, ikiwamo chakula bora ni muhimu kuzingatiwa.

"Utoaji wa huduma umekuwa ukitekelezwa kwa namna na viwango tofauti, baadhi ya wanafunzi wamekuwa wakinufaika, sasa serikali imeandaa mwongozo huu wa kisera, ili kuleta uratibu wa kitaifa ambao utanufaisha wanafunzi wote wa shule zote nchini,"alisema.

Alizitaka idara zote za serikali na wizara kuhakikisha zinasimamia utekelezaji wa mwongozo na kuhimiza wadau kusoma mwongozo na kila mmoja kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Alibainisha kuwa mwongozo huo umeweka utaratibu wa upatikanaji wa chakula, vyanzo vya upatikanaji wa chakula, mifumo ya uchangiaji, aina ya vyakula, mahitaji muhimu, wajibu na majukumu ya watekelezaji, ufuatiliaji na tathmini.

"Nitoe wito kwa wadau wote wa elimu kushiriki kuchangia utoaji wa chakula na lishe kwa kuwa suala hili ni mtambuka linahitaji ushirikiano ni matumaini yangu kuwa kila mmoja atasoma mwongozo huu na kutekeleza majukumu yote ipasavyo,"alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa PCI, Nicolas Ford, alisema shirika hilo lilitekeleza mpango wa chakula kwa elimu mkoani Mara, ambao umeonyesha mafanikio mbalimbali, ikiwamo kupunguza utoro na kuboresha mahudhurio kwa asilimia 89 kutoka asilimia 84.5 mwaka 2017.

Alisema mpango huo pia umesaidia kuongezeka kwa uelewa wa wazazi na kuongeza kiwango cha uchangiaji mazao ya chakula hadi kufikia tani 1,662 mnamo Septemba 2021.

Kamishna wa Elimu, Dk. Lyabwene Mtahabwa, alisema pamoja na juhudi za serikali za kuboresha miundombinu ya ujifunzaji na ufundishaji, hazitatoa matokeo tarajaji kama litasahaulika suala la upatikanaji wa chakula kwa wanafunzi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Stanslaus Nyongo, alisema Bunge linaunga mkono mwongozo huo na kutoa wito kwa wabunge na madiwani kuendelea kuhamasisha jamii kushiriki katika utoaji wa chakula shuleni.

Mwakilishi wa Balozi wa Marekani, Benjamin Mtaki, akitoa maelezo ya shirika la USDA, alisema Dola za Marekani milioni 67, zimetumika kwa miaka 10 kutekeleza Mpango wa Chakula kwa Elimu (FFE), ambao ulitekelezwa kwa awamu kuanzia mwaka 2010.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel (mwenye shati jekundu), akitoa maelekezo kwa viongozi wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), alipofanya ukaguzi wa miundombinu mbalimbali baada ya kuondolewa kwa wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga katika maeneo yasiyoruhusiwa, mkoani humo mapema wiki hii. **PICHA: ROSE JACOB**

# Wateja Vodacom M-Pesa kupewa gawio bilioni 5.1/-

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya mawasiliano ya Vodacom Tanzania, imeanza kutoa mgao wa Sh. bilioni 5.1 kwa watumiaji wake zaidi ya milioni 10, ikiwa ni sehemu ya faida iliyopatikana kwenye akaunti za M-Pesa.

Malipo haya yanatarajiwa kukamilika kesho, ambapo wateja wote watakuwa wameshapokea mgao wao.

Akifafanua kuhusu gawio hilo la M-Pesa, Mkurugenzi wa M-Pesa, Epimack Mbeteni, alisema jana kuwa: "Tuna furaha kubwa sana kuona kuwa pamoja na changamoto za mazingira ya biashara ambayo wateja wetu wamekuwa wakikabiliana nayo, huduma ya M-Pesa inaendelea kuwa msingi wa shughuli za kibiashara nchini.

"Tuko katika mchakato wa kugawa Sh. bilioni 5.1 kwa wateja wetu, ambao wamekuwa wakitumia mfumo wetu kwa kipindi hiki na malipo yanaingia moja kwa moja katika akaunti zao za M-Pesa."

Alisema faida italipwa kwa wateja, mawakala, wakala mkuu na wadau wengine wa kibiashara wa M-Pesa kulingana na matumizi yao ya huduma za M-Pesa.

Alifafanua kuwa gawio linategemea kiasi cha matumizi ya huduma katika kipindi hicho cha robo ya pili ya mwaka. "Shughuli hizo ni pamoja na kuhamisha pesa, kulipa bili, ununuzi wa muda wa maongezi na mengine.

"Kwetu Vodacom Tanzania, dhamira yetu ni kuhakikisha kuwa mfumo huu wa M-Pesa unaendelea kuwa mfumo unaoendana zaidi na mahitaji ya wateja," alisema.

Vodacom M-Pesa ni mfumo wa huduma za kifedha kwenye mtandao wa simu uliozinduliwa na Vodacom Tanzania Plc mwaka 2008.

Kwa sasa ukiwa umesajiliwa na shirika la GSMA na ukiwa na watumiaji zaidi ya milioni 10, mfumo wa M-Pesa umeongeza kwa kiasi kikubwa ushirikishwaji kifedha pamoja na shughuli za kiuchumi nchini.

Wateja wanaweka na kutoa pesa kutoka kwenye akaunti zao za M-Pesa kupitia mtandao wa mawakala Zaidi ya 108,000 nchi nzima.

Mtandao wa M-Pesa unaunganisha biashara, benki na taasisi za serikali katika kuwezesha miamala kidigitali.



## Shirika lashauri vyakula rutubishi

Na Augusta Njoji, DODOMA

SHIRIKA lisilo la kiserikali linalojishughulisha na masuala ya kuimarisha masuala ya lishe duniani (GAIN), limeshauri shule nchini kutumia vyakula vilivyorutubishwa ili kupunguza utapiamlo na udumavu kwa watoto.

Meneja Mradi wa Urutubishaji Vyakula kutoka Gain, Archard Ngemela, alitoa rai hiyo jana jijini hapa katika banda la maonyesho la shirika hilo kwenye uzinduzi wa Mwongozo wa Kitaifa wa Utoaji wa Huduma na Lishe Shuleni.

"Natoa rai kwa wenye shule kununua kwa wakulima nafaka zenye virutubisho na kuweka kwenye shule ili kusaidia watoto kukua kiakili na kimwili,"alisema.

Alisema serikali imejitahidi kuweka miongozo ya kuhakikisha vyakula shuleni vinakuwa vimerutubishwa.

"Mwitikio unaongezeka licha ya wengine walikuwa na mashaka na vyakula vinavyoongezwa virutubisho wakidhani kuna madhara katika afya, lakini kadri wanavyoelimishwa na kuhamasishwa wanaondokana na dhana hiyo,"alisema.

Ngemela alitoa wito kwa wadau kushiriki kuhamasisha kwenye shule ili wanafunzi wapate vyakula vilivyorutubishwa.

"Wazalishaji wako tayari kuchangia uzalishaji wa lishe shuleni kwa kuwa wanahitaji soko, kwa hiyo shule zikiweka mikakati kupitia kamati zinazohusika na vyakula wakahitaji vyakula vilivyorutubishwa kwa mujibu wa miongozo, uhitaji ukiwa mkubwa tutapata wazalishaji wengi na unga utazalishwa wa kutosha,"alisema.

Akizungumzia utekelezaji wa mradi wa masuala ya lishe Kanda ya Ziwa, meneja huyo alisema taarifa za lishe zilizotolewa na serikali zilionesha kuwepo na tatizo la utapiamlo na udumavu kwenye mikoa ya kanda hiyo.

"Moja ya virutubisho vinavyowekwa kwenye unga wa mahindi ni madini ya chuma ambayo yanasaidia kuongeza damu kwa wanawake wenye umri wa kuzaa,"alisema.

Alibainisha kuwa wamejipanga kwenda mikoa mingine kutoa elimu na kuhamasisha matumizi ya vyakula vilivyorutubishwa shuleni.

"Gain tunafanya kazi na wadau mbalimbali katika urutubishaji chakula, tunashiriki kuwawezesha katika virutubishi na kuwapa mafunzo ya uboreshaji, tunafanya kazi na TFNC katika kuhamasisha vyakula vilivyorutubishwa, tunafanya kazi na wadau kama Sanku katika utoaji wa mashine," alisema.

"Pia tunafanya kazi ya urutubishaji vyakula kibaiolojia. Tunashirikiana na wenzetu wa Harvest Plus, ili kupata virutubishi vingi muhimu kwa ajili ya watoto wetu shuleni," aliongeza.

Naye Ester Simfukwe kutoka Shirika la Harvest Plus, alisema wanashirikiana na Gain kuhamasisha matumizi ya mbegu na nafaka zenye virutubisho vingi hasa chuma na Vitamin A.

Alisema tayari wamefikia mikoa tisa kwenye kanda mbalimbali ambapo kuna mahindi na maharage yanapatikana kwa ajili ya mbegu na nafaka.

# Ummy azipa AZAKI kibarua madiwani

Na Augusta Njoji, DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imezitaka Asasi za Kiraia (AZAKI) kuwajengea uwezo madiwani kwenye halmashauri juu ya masuala mbalimbali ikiwamo usimamizi wa fedha na miradi ya maendeleo.

Waziri wa Nchi, TAMISEMI, Ummy Mwalimu, aliyasema hayo juzi alipokuwa akifunga wiki ya AZAKI iliyofanyika jijini hapa huku akisema hatua hiyo itasaidia kujisimamia kwenye shughuli zao za kimaendeleo na kiuchumi.

"Napenda kuwapongeza sana kwa elimu mnayotoa kwa wananchi kwa kuwajengea uwezo. Lakini naomba mwende mbali zaidi kuyafikia mabaraza ya madiwani kwenye halmashauri zetu ili nao wajengewe uwezo wa kusimamia halmashauri kwenye matumizi ya fedha na ufuatiliaji wa shughuli za maendeleo,"alisema.

Aidha, Waziri Ummy alisema serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa mshirika hayo na kuyasihi kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi ili kuchangia maendeleo ya nchi.

"Kwa kutambua mchango wa AZAKI, natoa wito kwenu kuendelea kushirikiana na kuihudumia jamii ambayo Asasi hizi mmekuwa mkifanya kazi ni zuri kwa kuifikia jamii hasa wananchi walioko vijijini kwa kushirikiana na Serikali za Vijiji na halmashauri,"alisema.

Hata hivyo, alitoa wito kwa sekta binafsi kuwekeza kuchangia ukuaji wa maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla.

Awali, Mratibu wa Wiki ya Azaki na Mshauri wa Foundation for Civil Society (FCS), Justice Rutenge, alibainisha kuwa katika wiki hiyo kumekuwapo na mijadala mbalimbali iliyowakutanisha wadau wa asasi , Wabunge, Makundi Maalum na wananchi na ililenga kujadili masuala yanayohusu ustawi wa nchi na maendeleo ya taifa.

"Mwaka huu wiki hii imekutanisha zaidi ya AZAKI 300 kuanzia siku ya ufunguzi na baadaye kushiriki kwenye mijadala mbalimbali iliyowawezesha kutoa mawazo yao juu ya masuala mbalimbali ya ustawi wa jamii na taifa kwa ujumla,"alisema.



Imamu wa Msikiti wa Nughe, jijini Dodoma, Omari Salumu (kushoto), akikabidhi msaada wa vitu mbalimbali kwa mgonjwa Aziza Yusufu aliyelazwa wodi ya kinamama katika Hospitali ya Rufani ya Dodoma jana, ambapo zaidi ya wagonjwa 400 walinufaika na msaada huo. PICHA: IBRAHIM JOSEPH

# Mpango kutambua wagonjwa TB kwa 75%

Na Renatha Msungu, DODOMA

MPANGO wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma (NTLP) umejipanga kuwatambua wagonjwa wa kifua kikuu ili kupata matibabu mapema na kupunguza vifo vitokanavyo na ugonjwa huo kwa asilimia 75.

Meneja wa Mpango huo, Riziki Kisonga, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye tamasha la Dodoma lililojumuisha taasisi mbalimbali za afya.

Alisema hadi sasa mpango huo umewatambua wagonjwa kutoka asilimia 45 kwa mwaka 2015 hadi asilimia 64 kwa mwaka 2020.

Kisonga alisema idadi ya wagonjwa wa TB kidunia ni milioni nane huku Tanzania wakiwa 173,000 ambao wanatambulika.

"Kulingana na takwimu hizo tunajitahidi kuhakikisha wagonjwa wote tunawafikia na kuwapa matibabu,"alisema Kisonga.

Alisema kwa sasa kuna kliniki tembezi tano ambazo zimegawanywa katika Kanda tano na zinatembea kwenye mikoa ili kutoa elimu na kuwafikia wagonjwa.

"Tayari tumewafikia wagonjwa wa kifua kikuu hapa nchini kwa asilimia 95 ni hatua kubwa sana kwa kitengo hiki na kuongeza kuwa wanahitaji kufikia asilimia 100 ili kuukabili ugonjwa huu," alisema. Alitoa wito kwa wananchi kuhakikisha wanajitokeza kutibiwa ugonjwa huo kwa sababu mgonjwa mmoja wa kifua kikuu ana uwezo wa kuambukiza watu 20 kwa wakati mmoja.

Kuhusu ugonjwa wa ukoma, meneja huyo alisema wamepanga hadi kufikia 2030 kuwa wametokomeza ugonjwa huo.

Kwa upande wake, Waziri wa Afya, Maendeleo yua Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alisema jamii inapaswa kujitokeza kupima ugonjwa huo kutokana na kuambukiza kwa haraka.





# Chanzo wabunifu kukosa fursa bayana

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KUKOSEKANA kwa eneo maalum la kuwaendeleza wabunifu katika ujasiriamali, kumesababisha wabunifu vijana kupotea na kutotimiza malengo yao visiwani Zanzibar.

Hayo yalisemwa juzi na Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Kuendeleza Viwanda Vidogo na vya Kati Zanzibar (SMIDA), Soud Said Ali, wakati akitangaza washindi wa shindano la ubunifu katika kilele cha maadhimisho ya miaka 76 ya Umoja wa Mataifa (UN) kwenye ukumbi wa Sheikh Idris Abdulwakil, Kikwajuni Zanzibar.

Alisema sekta ya ubunifu inakabiliwa na vikwazo vingi, ikiwamo kutokuwa na sehemu ya kuwaendeleza wabunifu na baada ya kufanya ubunifu, hupotea na taasisi mbalimbali kutokuwa na taarifa rasmi kuhusu kuwapo kwao.

Hatua hiyo alisema imesababisha wabunifu walioibuliwa kuvunjika moyo kuendeleza kazi za ubunifu.

Kutokana na hali hiyo, alisema SMIDA inaandaa mpango wa kuwaendeleza wabunifu na kukuza ubunifu wao, ili kusiadia nchi katika uchumi.

"Kwa hatua hizo wabunifu wetu watajikwamua kiuchumi, ili kuendeleza taifa likiwa na vijana wenye uvumbuzi hasa katika uzalishaji, TEHAMA (Teknolojia ya habari na mawasiliano), uchumi wa bluu na kuifanya Zanzibar kuwa kitovu cha biashara," alisema.

SMIDA, alisema imeanza mazungumzo kupitia Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha anaeshughulika TEHAMA, ili kuandaa mpango wa kuwaweka pamoja wabunifu, ili Zanzibar kuwa kituo cha kutoa huduma tofauti duniani katika teknolojia.

Mshindi wa kwanza katika shindano hilo, Hamid Abdallah Wailu, aliyebuni mfumo wa upimaji wa mafuta ya taa, petroli na dizeli katika matangi ya kuhifadhia mafuta, alisema mfumo huo utaepusha ajali za moto ikiwamo milipuko katika vituo vya kuhifadhia mafuta.

Pia alisema mfumo huo utaonyesha ongezeko la joto kwenye matangi hayo na kuwezesha kufungua mfumo wa upumuaji, ili kupunguza joto sambamba na kujua kiwango cha mafuta kinachoingia na kuuzwa katika soko.

"Mfumo huu mbali ya kupunguza ajali za moto katika bohari na vituo vya mafuta, pia utaweka udhibiti wa taarifa zinazohusiana na mafuta yanayoingia nchini kwa wadau popote alipo," alisema Hamid.

Naye Barke Ukusi, aliyeshika nafasi ya pili katika shindano hilo kutokana na kuvumbua mfumo wa kufuatilia mwenendo wa samaki na utoaji wa taarifa za ajali baharini uitwao 'Samaki Mtandaoni', alisema mfumo huo utasaidia kutatua matatizo ya wavuvi na kuongeza tija na ufanisi kwenye kazi zao.

"Mfumo huu utaondoa changamoto ya wavuvi kuvua kwa kubahatisha na kutoa taarifa kwa wakati inapotekezea ajali na kupata msaada wa haraka, pia mfumo utakuwa na kifaa cha kuvutia samaki," alisema.

Kwa mujibu wa Barke, amevumbua mfumo huo kutokana na wavuvi kukosa soko la kuuzia samaki na kutokuwa na maendeleo hasa ikizingatiwa kuwa wavuvi wengi kipato chao ni kidogo, hivyo mfumo wa samaki mtandaoni kutawezesha watu kununua samaki kupitia mtandaoni.

Alisema changamoto inayowakabili wabunifu Zanzibar ni kutokutambulika serikalini, hivyo kusababisha ubunifu wao kufifia na hatimaye kukata tamaa.

Kutokana na ubunifu huo, Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi, aliwapongeza vijana hao kwa ubunifu na kuahidi kuwa serikali itatengeneza eneo maalum la vijana kufanya ubunifu na kuhakikisha serikali inawasadia vijana hao.



Mkuu wa Wilaya ya Kalambo, mkoani Rukwa, Tano Mwera (kulia), akizungumza na Maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), waliofika wilayani humo jana, kwa ajili ya kufanya kampeni ya utoaji elimu kwa mlipakodi, mlango kwa mlango. **PICHA: TRA**

# Waziri aagiza uchunguzi moto hotelini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Leila Mohd Mussa, amelitaka Jeshi la Polisi Mkoa wa Kusini Unguja na Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) kuharakisha kufanya uchunguzi wa kujua chanzo cha moto katika hotel ya Arabian Night, Paje Mkoa wa Kusini Unguja.

Leila aliyasema hayo jana alipofika hotelinui hapo kwa lengo la kuangalia athari iliyojitokeza na kutaka kujua chanzo cha moto huo, ambao umesababisha hasara kubwa.

Alisema serikali inathamini uwapo wa wawekezaji nchini na wanachangia asilimia kubwa pato la taifa, hivyo itahakikisha mmiliki wa hoteli hiyo anapata haki yake, ili kuendelea na shughuli za ujenzi.

Naye msimamizi wa ujenzi wa hoteli hiyo, Khamis Mahadhi Mohd, aliishukuru serikali kwa kuthamini uwapo wao na kuiomba kusogeza huduma za uzimaji moto hasa katika maeneo ya hoteli. "Tunaiomba serikali kuwa na kituo cha zima moto na uokozi katika hoteli za kitalii, ili kuokoa mali kwa wakati pale maafa yanapotokea," alisema.

Meneja Uhusiano wa Benki ya CRDB anayeshughulikia bima, Hamida Juma, alisema hatua za awali zimeshafanyika na kuahidi kumpatia fidia mara tu uchunguzi utakapokamilika.

Chanzo cha moto huo pamoja na gharama ya vitu vilivyoungua bado haijajulikana. Moto huo umeteketeza vitu mbalimbali., likiwamo paa la hoteli na baadhi ya vifaa vilivyokuwamo hotelini.

## Benki yasisitiza uamuzi sahihi katika ujenzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MENEJA wa Uhusiano wa Benki ya NCBA, Mulindwa Tishekwa, amesema ujenzi wa aina yoyote unahitaji uamuzi sahihi, ambao unawezeshwa na taarifa za kutosha ikiwamo namna bora ya kupata usaidizi wa kifedha, ili kukamilisha kilichokusudiwa.

Akizungumza hivi karibuni katika maonyesho ya nyumba (Home Expo Zanzibar) yaliofanyika mjini Zanzibar, alisema NCBA inaamini kuwa kila mtu anayo fursa ya kuishi kwenye nyumba bora, haijalishi ana kipato cha aina gani.

Tishekwa alisema benki hiyo ina rasilimali za kumwezesha kumiliki nyumba kwa kukopa na kulipa kidogo huku akiendelea na shughuli zake za maisha ya kawaida.

"Nchi inatakiwa kuwa na miundombinu ya kisasa, ili kuwawezesha wananchi wake kuzifikia huduma mbalimbali za kila siku kwenye maisha yao. Kwa hiyo, tunakaribisha kampuni na watu wenye miradi ambayo inahitaji usaidizi wa kifedha," alisema.

Alisema kuwa benki hiyo ikiwa ni taasisi ya kifedha, inayo wajibu wa kuhakikisha wananchi wananufaika na huduma wanazotoa pamoja na kuchangia ujenzi wa taifa.

Pia alisema maonyesho hayo ni muhimu kwa ukuaji wa sekta ya ardhi, hivyo ni vyema yakafanyika kila kona ya nchi na fursa bado ni kubwa kwa maendeleo ya wananchi.

Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi Zanzibar, Riziki Pembe Juma, alisema matumizi bora ya ardhi yana lengo la kuleta misingi imara na malengo ya maendeleo endelevu ya Zanzibar.

Aidha, alisema maonyesho hayo ni mwanzo katika kutangaza fursa za makaazi ndani ya Zanzibar hivyo wananchi wana kila sababu ya kujipongeza na kufurahia jambo hilo.

Alisema kabla ya Mapinduzi ya mwaka 1964 wananchi walikuwa wakiishi katika nyumba zisizo na ubora zilizojengwa kwa nyasi na zingine kwa mawe, lakini baada ya Mapinduzi, wananchi waliishi katika nyumba za kisasa.

Pia alisema maonyesho hayo ni fursa muhimu kwa wadau wote wakiwamo wazalishaji wa bidhaa viwandani na wadau wengine kuwekeza Zanzibar.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI OKTOBA 30, 2021



DADA 'AKE BURNA BOY AUPIGA MWINGI Ukurasa.14



# Kweli Isha, mganga haagizi tembele

"SIWEZI kumaliza kuku, wala kuvunja nazi njia panda kwa sababu ya kuolewa. Ndoa ni majaliwa." Ni maneno ya staa wa muziki wa taarabu, Isha Mashauzi.

Msanii huyu ambaye amepitia makundi mbalimbali, mpaka sasa kuwa na kundi lake la Mashauzi Classic, anasema pamoja na kwamba mpaka sasa hajaolewa, lakini anaishi kwa amani na kinachompa furaha kitabaki kuwa moyoni mwake.

"Kuolewa ni majaaliwa. Kuna watu wanatembea mpaka yeboyebo zinakuwa kama opena za baa, hajawahi kuambiwa hujambo hata na nzi," anasema mwimbaji huyo na kuongeza.

"Waganga hawaagizi samaki, dagaa wala tembele. Wanaagiza kuku tu. Hivi umeshawahi kumuona mke wa mganga wa kienyeji mwembamba? Mwenyewe mganga ni mwembamba, lakini siyo mkewe. Sababu ni wale kuku wanaoletwa na wateja zao. Mimi kama Mungu amepanga sawa nitaolewa, lakini siwezi kulazimisha kwenda kwa mganga wa kienyeji, sitaki kujidhalilisha. Maana unaweza kufanya hayo yote, Mungu akakupa mume mwenye mtihani kwa sababu umelazimika." Anasema.

Si kwamba hajawahi kuolewa, anasema alikuwahi kuwa kwenye ndoa mwaka 2000, lakini wakati ule alikuwa na umri mdogo sana na utoto ndiyo uliomfanya kuachika.

"Mume wangu alikuwa na mke mwingine, sasa mimi nilikuwa nataka alale kwangu tu, hata zamu ya mwenzangu. Kusema kweli sikupenda mitala. Ila baadaye nilijuta kwa sababu niligundua ilikuwa ni haki ya kila mmoja. Narudia tena ni akili za kitoto.

Niliachwa kwa talaka tatu na mwaka 2005, ndipo nilipoanza mambo ya muziki.

Anasema jirani na alipokuwa anaishi kulikuwa na ofisi za Jumuiya ya Wazazi, Siza Mazongela na kundi lake la Tandale Modern Taarab, walikuwa wanafanya mazoezi. Siza ni mwimbaji maarufu wa nyimbo za Kizaramo na wimbo maarufu uliovuma wakati huo ni 'Shaaban Madobe'.

"Nilikwenda na nikamwambia mimi naweza kuimba. Nikajaribiwa nikaweza na hapo ndiyo ikawa mwanzo wa safari yangu ya muziki." Alisema.

BASI SAWA

## Konde yupo High School

DU! Mjini kuna mambo. Hutakiwi kukosa bando. Yule mkali wa bongo fleva, Harmonize, baada ya Ali Kiba kutoa albamu yake aliyoiita 'One Only King', akaona isiwe tabu. Na yeye amefyatua albamu yake mpya ambayo ameipachika jina la 'High School'.

Hii ina ngoma 20 kali, ambazo mashabiki wake watakuwa wakichizika nazo.

Ndani ya albamu hiyo kuna mikwaju ya adabu kama vile 'Sorry', 'Out Side', 'Serious Love','Always', 'Why', 'Turn Up', 'Usia', 'Mtaje', na 'Dunia'.

Ngoma zingine ni 'Mdomo', Infiencer', 'Mood', 'Single', 'What do you Miss', 'Ichant Stop', 'One Quetion', 'Sadakalawe', 'Muziki', 'Kamaliza' na 'Teacher.'



## Nature umekipiga na Boban? Unatisha

KUMBE bwana, Juma Nature kama asingekuwa msanii wa bongo fleva na hip hop, angekuwa mchezaji mkubwa tu hapa nchini.



Keshakipiga na wachezaji ambao walikuwa mastaa wakubwa nchini, Haruna Moshi 'Boban' na Athumani Chuji ambao kwa sasa hawachezi soka la kiushindani. Ni mmoja tu ambaye anacheza Ligi Kuu, Kelvin Yondani.

"Baba alinikataza kucheza mpira, yaani umaarufu wangu kama usingekuwa kwenye muziki, basi ungekuwa kwenye soka. Mimi ni bonge la straika, nimecheza na kina Yondani, Boban na Chuji, wenzangu wamekuwa mastaa kwenye soka, mimi dingi akasema yaani chakula nikutafutie mimi, halafu wewe unakwenda kucheza mpira, huo ujinga sitaki, tafuta kazi nyingine na hii yote kwa sababu niliumia mbavu kwenye mechi," anasema Nature.

Akasema baada ya hapo aliingia rasmi kwenye muziki, baada ya kuachana na mambo ya soka. Anasema mpaka sasa bado ana nguvu za kucheza soka, lakini alishaacha zamani.



## Ndoa ya Hamisa Mobeto kweli au kamba?

MMEMSIKIA DC wa Instagram, Mwijaku? Anasema kuwa staa, mwanamitindo na mwimbaji, Hamisa Mobeto ataolewa mwakani.

Anamtaja mume mtarajia hatoki Bongo wala Afrika. Mwijaku ambaye anadai kuwa ndiye kaka wa Hamisa anasema ndoa hiyo itafanyika bila kukusanya michango kutoka kwa mtu yeyote yule na MC atakuwa mwenyewe.

"Halina ubishi, Hamisa ndiyo mwanamke mrembo zaidi nchini Tanzania. Atakayemuoa si Mtanzania, anatoka Ulaya wala siyo Afrika. Na harusi haina mchango." anasema Mwijaku.

Haya wazamiaji, sherehe za harusi hizo, hazina michango, wala kadi, siku hizi mifuko ya rambo hakuna, sijui mtabeba nini?




## Mji wa laana: Mzee mpenda wasichana

Na Adam Fungamwango

MAPENZI ni kuridhiana na si kulazimishana. Hata kama msichana akimpenda mwanaume mtu mzima,hakuna tatizo kama wameridhiana. Tatizo linakuja pale kulazimishana. Kuna baadhi ya watu wazima, wanapokuwa na madaraka, vyeo, utajiri au nguvu fulani kwenye jamii, hutumia kujinufaisha kwa kulazimisha mapenzi kwa wanawake, hata kama hawajaridhia kuwa naye.

Siku zote mapenzi ni mapenzi tu. Hata mtu awe na cheo, pesa, mamlaka na umaarufu, lakini bado huwezi kununua penzi. Utakachonunua ni ngono tu.

Kwenye filamu ya 'Mji wa Laana', kuna mzee mmoja anaitwa mzee Mweleka. Huyu amerithishwa nguvu za ajabu na babu yake. Badala ya kuzitumia kunufaisha wananchi wa kijiji, yeye anazitumia kwa manufaa yake na kuua watu wengi, kiasi cha kuogopwa kama ukoma.

Imechezwa na wasanii Said Ndimbwa, Hassa Danty, Mary Lazaro, Bahati Sharifu, Nasma Hamisi na wengineo.

Mzee Mweleka anafanya kazi ya kuona wasichana wadogo bila ridhaa yao. Wanakubali kwa sababu ya hofu ya kuuawa. Mbaya kuliko zote ni kwamba mtu yoyote mwenye mke kwenye kijiji au mji huo, kuna siku mkewe anakwenda kulala kwa mzee huyo. Na hiyo ilikuwa ni lazima, sivyo mume anakufa. Wanaume wengi waliridhia kwa sababu baadhi yao waliuawa kwa nguvu za kishirikina na mzee huyo.

Mary, msichana mrembo anayechipukia, anaonekana na mzee huyo ambaye tayari alikuwa ameshajipachika ufalme kwenye kijiji hicho. Mzee akakolea na kutaka kumuoa. Mary akakataa kwa madai ana mchumba wake. Kwanza mchumba huyo anakufa kifo cha ajabu. Halafu mwanaume yeyote aliyejitokeza kumkumbatia Mary anauawa. Hasira za mzee Mweleka kumkosa Mary, anasababisha mtu yeyote akinywa maji kwenye kijiji hicho anafariki. Wananchi wakalazimika kwenda vijiji vya jirani. Habari zinatapakaa.

Anafika mgeni kwenye kijiji hicho asiyejulikana. Anafikia kwa kijana Mwanjoke ambaye mpenzi wake yupo kwa Mweleka. Anamsimulia yote. Anapita Mary, mgeni ambaye jina lake Chiote anampenda. Anambusu. Hakuna kilichotokea, Mary anashangaa kwani aliona laana ya vifo vya wanaume, wanambusu imepotea.

Kumbe mgeni yule ndiye mkombozi, alikuja kuwakomboa wanakijiji kwa sababu alijua nguvu zote za mzee huyo ziko wapi. Alikwenda nyumbani kwake, anamvua kofia na pete. Mweleka nguvu zikamuishia. Akabaki kama raia wa kawaida. Kila msichana akarudi kwa mpenzi wake, wake za watu wakarudi kwa waume zao. Mgeni Chiote akajichukulia Mary wake.





## Aunt Ezekiel unatuchanganya ujue?

KUNA picha zimetrendi hivi sasa zikionyesha kuwa mlimbwende wa zamani na mwigizaji wa bongo movie, Aunt Ezekiel alionekana yuko kwenye vazi la harusi, akifunga ndoa na mpenzi wake Kusah.

Lakini mwenyewe ameshindwa kuweka wazi kama ilikuwa ndoa au la.

"Wao inawahusu nini? Tufunge tusifunge inawahusu nini. Mimi nadhani hicho ni kitu ambacho hawatakiwi kujaji sana. Iwe kweli au siyo kweli ni maisha yetu sisi." Anasema Aunt.

Wakati bibie huyo akishindwa kuweka wazi kama ile ilikuwa ndoa au la ni picha tu, alichoshindwa kukificha ni hisia zake juu ya mpenzi wake huyo.

"Napenda kumwambia kuwa nampenda sana."

Kusah mwenyewe naye akasema kuwa anampenda sana Aunt Ezekiel na anamheshimu.

"Amenipa vitu ambavyo siwezi kuvirejesha. Itoshe kusema kuwa nampenda sana," anasema.

Anasema kuwa kwa kipindi kifupi ambacho ameishi naye amepitia vitu vingi.

"Ni mwanamke wangu, shujaa wangu, namkubali sana." Kusah huyo.

## Usaliti mapenzi ulikuwepo toka 'longi'

Na Adam Fungamwango

NANI kasema eti siku hizi ndiyo kuna usatili wa mapenzi? Kumekuwa na dhana kuwa kizazi cha sasa ndicho kimezidi kwa kufanya usaliti, si wanawake wala wanaume.

Lakini ukitaka kujua sivyo, hebu fuatilia nyimbo za miaka ya nyuma. Nazo zilikuwapo za usaliti. Mwanamuziki na msanii ni kioo cha jamii. Anachokiimba au kukitoa ndiyo kipo kwenye jamii kwa wakati huo. Kwa maana hiyo kama kuna nyimbo za zamani ambazo wanamuziki wanaimba kuhusu usaliti wa mapenzi, ina maana huko miaka ya nyuma jambo hilo pia lilikuwapo.

Kwa ushahidi hapa tutaangalia nyimbo tano tu, ambazo wanamuziki wanalalamika juu ya kusalitiwa kimapenzi.

### KUPATWA KWA MWEZI-MWENGE JAZZ

Bendi inayomilikiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), katikati ya miaka ya 1980, walifyatua wimbo ulioitwa 'Kupatwa kwa Mwezi'. Ni wimbo unaomzungumza juu ya usaliti.

Baba anambembeleza binti yake na kumwambia anyamaze. Binti mdogo analia kwa sababu mama yake ametoroka nyumbani na hajulikani alipo.

Baba anamwambia mama yake ametoroka baada ya kumpata bwana mwingine ambaye ana pesa nyingi zaidi yake. Anamwambia avumilie kwani siku si nyingi atampata mama mwingine.

Anakwenda mbali zaidi kwa kusema alipokuwa na mali nyingi, mke alimuoa kama 'mungu wa pili', lakini aliposimamishwa kazi, akageuka, akamfilisi mali yote, akamtoroka.

### FARIDA-TABORA JAZZ BAND

Ilikuwa ni miaka ya katikati ya 1970, wakati Tabora Jazz, walipoachia kibao kiitwacho 'Farida'.

Jamaa alimchukua demu akiwa choka mbaya huko Mwanza, akaenda naye Dar es Salaam. Jiji la raha na karaha. Alipoanza kupendeza tu, tabu ikaanza. Alipokwenda safarini Tanga na kurudi hakumkuta Farida nyumbani. Kama haitoshi, demu anakomba kila kitu na kumuacha mweupe kama unga wa sembe. Mara nyingi waimbaji wa zamani walikuwa wanaimba vitu ambavyo ni kweli vimetokea.

### CHENGA YA MWILI-DDC MLIMANI PARK

Mwishoni mwa miaka ya 1980 na mwanzoni wa miaka ya 1990, DDC Mlimano Park walitoa wimbo ya 'Chenga ya Mwili'. Ni kisa kinachohuzunisha.

Jamaa aliletewa mtu nyumbani kwake ikidaiwa ni mjomba wake. Aliyemleta ni mchumba wake ambaye walikuwa wanaishi wote, lakini kwa ahadi ya kufunga ndoa.

Aliambiwa nyumbani kuna matataizo, hivyo wanaondoka na mjomba wake kulitatua. Wakati wanamuacha Uwanja wa Ndege, aliona wanakumbatiana na kuingia ndani ya ndege. Ndipo alipogundua amepigwa chenga ya mwili. Yule alikuwa na mpenzi wake.

### NENDA UKAISHI SALAMA-UDA JAZZ BAND

Mtunzi marehemu Mikidadi Seif alisema hili ni tukio la kweli lililomtokea mwenyewe miaka ya 1980. Mke wake walimtoroka na kwenda kuishi na rafiki yake. Kwa uchungu ndipo alipotunga na kuimba wimbo huu.

### MAYA-MAFUMU BILAL

Marehemu Mafumu Bilal alitunga na kuimba wimbo wa 'Maya'. Ni jamaa anayelalamika kusalitiwa na mkewe.

Tena kwa mtumishi wa ndani 'hausi boi' ambao ndiye akageuka bwana.

Haya mambo yalitokea zamani sana. Yanaendelea na yataendelea. Kwa sababu dunia ndivyo ilivyo.


MAFUMU BILAL



# Dada 'ake Burna Boy aupiga mwingi

FAMILIA ya nyota wa muziki kutoka nchini Nigeria, Burna Boy imeendelea kutrendi baada ya mdogo wake wa mwisho wa kike, Nissi Ogulu kuhusika kwenye uundaji wa gari aina ya Range Rover toleo jipya la mwaka 2022.

Kupitia kurasa zake za mitandao ya kijamii ameonyesha furaha yake ya kuwa sehemu ya timu iliyohusika kukamilisha gari hilo ambalo wametumia miaka mitatu kuliunda.



## Sankara apeleka Kiswahili Canada

WAIMBAJI wanne wenye asili ya Congo DR, waishio nchini Canada wameunganishwa na lebo ya VL Production, ili kutoa burudani kwa Kiswahili kama njia mojawapo na kutangaza lugha hiyo nje ya mipaka ya Tanzania.

Mwanzilishi wa lebo hiyo, Thomas Sankara, amewataja waimbaji hao kuwa ni Aeli G, Djed Banks, Noir na Wed Wedundu, kwamba malengo ya lebo hiyo ni kukuza Kiswahili na vipaji vya vijana nchini humo na duniani kwa ujumla.

Amesema, kwa sasa Kiswahili kinazidi kupata umaarufu mkubwa katika nchi mbalimbali duniani, hivyo na yeye ameona atumie lebo yake kusaidia kukitangaza kupitia muziki.

## Janemena sasa unajua umuhimu wa mume

MNENGUAJI maarufu Janemena ameamua kuweka wazi kwamba sasa anajua kwa nini baadhi ya wanawake hawataki kuwatambulisha wanaume zao mitandaoni.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, amesema kuna wanawake wenye uchu, ambao wanasubiri wanaume kutambulishwa ili kuwabeba.

"Kila mwanamke hataki kumuonyesha mume wake katika mitandao ya kijamii, hii inatokana na tabia ya wanawake wenye uchu kuwabeba na kuwaachia vilio" amesema.





## Zlatan hongera kwa unalomfanyia

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Zlatan Ibile, amefanya maajabu baada ya kumzawadia mwanasheria wake Gari jipya LA kifahari.

Mkali hiyo wa kuziki, aliweka ujumbe na picha ya Gari katika ukurasa wake wa Instagram, akisema hiyo ni zawadi yake ndogo kwa mtu wake muhimu.

"Nadhani ni mwanasheria wa kushangaza, kila wakati unanifanyia mambo mengi chanya, Nina uhakika hii inakufaa," ameandika Zlatan.

## Zayn huwezi kumuumiza mama mkwe

MWANAMUZIKI wa Marekani Zayn Malik, anashikiliwa na polisi kwa tuhuma ya kumshambulia mama mkwe wake Yolanda Hadid.

Kulingana na mtandao wa TMZ, msanii huyo nyota amemshambulia mama wa mpenzi wake Gigi, kwa kumchoma na kumsababishia maumivu makali.

Malik imearifiwa alijisalimisha baada ya shambulizi hilo lililotokea katika ranchi ya mwanamke huyo huko Pennsylvania.



MAKALA

## ILIVYOKUWA ZAMANI, LEO NA YAJAYO...

# Namna ulivyokuwa usafiri nchini na safari ndefu maisha yalikotoka

**Na Adam Fungamwango**

WIKI iliyopita safu hii ilikuwa na simulizi ya namna makazi yalivyozoa umaarufu majina, hata kugeuka ubatizo wake maalum hadi sasa, jijini Dar es Salaam.

Je usafiri nao ukoje? Kuna msemo 'tumetoka mbali.' Ni nchini kote kila magari yaliyotamba yalikuwa ya aina kadhaa, kwa magari madogo mitaa ya mijini na vijijini ilishikwa na magari madogo aina ya Landrover 109, ambayo ilishika ofisi zote za serikali na wanausalama.

Magari madogo ya kawaida yalitekwa hasa na aina ya Peugeot, kuanzia na aina 403, katika miaka 1960 hadi mwanzoni mwa miaka 1970.

Toleo la kwanza lilikuwa na milango yake inayofungika kinyume na mwelekeo wa milango ya magari ya sasa. Baadaye zikaja Peugeot 404, ambazo zilidumu miaka mingi kutamba na kwa kiasi kikubwa teksi mijini.

Kutamba kwa muda huo, ikapinduliwa na aina ya 504, ambayo watu maarufu na 'mapedeshee' ndio walitumia kujidai nazo. Kuna wakati ziliingizwa kwa wingi nchini, za pekee ambazo kwa juu ilikuwa na sehemu ya kufunua na usukani mkono wa kushoto.

Kuna wakati serikali ilichukua hatua kukamatwa magari hayo ambayo yalipewa majina 'magari mtumba' jijini Dar es Salaam, zilikuwa nyingi sana zimekusanywa iliko Uwanja wa Taifa sasa, zama hizo zikiwa uwanja wa wazi na palitumiwa na watu kujifunzia uendeshaji magari.

Baadaye zikatoka Peugeot 204, kisha 505, 305, kabla ya soko kuvamiwa na Wajapani na wenye Peugeot kutoweka nazo nchini, kutoka ofisi zake zilizokuwa mkabala na iliko hoteli Serena, Dar es Salaam.

Gari aina nyingine zama hizo zilizotamba, yalikuwapo magari aina ya Ford Escort kutoka Marekani, zilizotamba kuanzia mwishoni miaka mwa miaka 1969, ambazo zilitikisa mitaa ya baadaye ni aina ya Ford Cortina.

Hizo zilikuwa maarufu kwa huduma ya teksi zilitamba mitaani, hapo jijini Dar es Salaam kunakumbukwa teksi gari aina hiyo iliyoitwa 'Safari na Muziki; maana ilikuwa na waya mrefu wa radio na muziki 'unadunda' ndani.

Kikubwa kingine kwa gari hilo ambalo kituo chake kilikuwa Temeke mkabala na iliko sasa Kituo cha daladala Temeke Hospitali, ingawaje liitamba mji mzima, dereva wake alikuwa shabiki mkubwa wa klabu maarufu wa soka ya jijini, hata kufikia kuweka rehani kwa mfano wa kubeti sasa, kuhusiana na matokeo ya mechi za vilabu Simba na Yanga, pale zilipopambana.

Aina nyingine za magari zilizotamba wakati huo, ni Mercedes Benz, zaidi zikimilikiwa na serikali kwa ajili ya viongozi wakuu, huku matajiri nao walionekana kuwa nazo. Hadi sasa hiyo haijatakea katika milki ya magari aina ya Benzi.




Basi lililomilikiwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC), zama hizo.

**MABASI JE?**

Usafiri wa jijini daladala za leo nao una mzizi mrefu. Ni tangu uhuru hadi kufika katikati ya miaka ya 1960, ambayo kulikuwapo mabasi yaitwayo DMT, kwa maana 'Dar es Salaam Motor Transport.'

Ni aina ya mabasi ambayo yalidumu kati ya miaka ya 1970 DMT ikagawanywa katika pande mbili, moja Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) lililoko jijini Dar es Salaam na mwa safari ndefu Ikaundwa, Kampuni ya Mabasi ya Umma (KAMATA).

Hilo likaumbana na mabasi ya safari ndefu, mali ya Shirika la Reli Tanzania (TRC), ambalo lilitoa huduma kufika maeneo ambako hakuna reli, mathalan mikoa ya Kanda za Juu Kusini.

Kulishuhudiwa safari aina yake mabasi kati ya Dar es Salaam na Kyela mkoani Mbeya kuchukua siku mbili, inapotoka Dar es Salaam, usiku wa manane inakuwa Mikumi na asubuhi Iringa.

Kote hapo inaposimamiwa inakagulwa kiufundi na kuichukua muda usiopungua saa moja na nusu au zaidi.

Kimsingi, hadi kufika Kyela ilifika usiku siku ya pili tangu ianze safari na kwa walioekelea umbali kama Sumbawanga ilikuwa maradufu, ndivyo ilivyokuwa safari za wakati huo wa TRC, vivyo hivyo kukawapo yanayoshabihiana na ule wa KAMATA.

Kwa binafsi yanayoelekea miji ya Bukoba yalivuka nchi jirani ya Kenya, kisha Uganda na kutokea Mutukula hadi Bukoba mjini, huku yaendayo Musoma alipita Kenya na kutokea mpakani Tarime.

Leo hii safari iliyochukua zaidi ya saa 24 wakati huo, sasa nchi chini ya saa 12. Mabasi mjini, nako daladala tangu mwanzo wake na mabsi aina ya Leyland Albion katika miaka ya 1960, iliyopita mageuzi mengi, ikianzia na mabasi aina Leyland Albion na kupitia Leyland aina tofauti, hasa kuna wakati zikatoka aina mpya za Leyland zikitumia mali ya UDA, baada ya DMT kuvunjwa na kuzaliwa KAMATA na UDA.

Hapo kwa na mvuto ambao yaweza kuwa kichekesho "imenunuliwa nusu milioni, endesha kwa umakini' ndivyo aliyoandikwa dereva chini ya usukani wake.

Haikuchukua muda mrefu, yakaanza kutolea aina mpya nchini, mabasi na malori aina mbalimbali zilizotamba, kama vile Scania 82 nba Scania 101.

Mwanzoni kabisa mwa miaka 1980, kukawapo mabasi ambayo yalikuwa yanatoa huduma kwa 'kuiba ruti' yakitoza bei shilingi tano ikiwa juu sana kwa nauli ya kawaida, miaka michache baadaye ikaruhusiwa kwa jina walilopewa katika 'kuiba ruti' la 'daladala; mapema kabisa ya mwaka miaka 1980, kwa msukumo wa peke Waziri Mkuu Edward Sokoine, na ndio imedumu nayo hata baada ya kuipiku UDA katika soko.






Picha juu, liliilokuwa basi la Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) na chini, daladala wakati huo maarufu kwa jina la 'Chai Maharage'. Aina hizo za daladala zimeshatoweka jijini. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**SIMULIZI ZAIDI JUMAMOSI**

# Nyota ya Rais Samia inavyong'aa katika usawa wa uchumi kijinsia

Na Mary Geofrey

MNAMO Septemba 23, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, alihutubia Mkutano wa 76 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UN), New York nchini Marekani.

Katika mkutano huo, Rais Samia ameeleza jitihada za serikali nchini kuongeza ushiriki wa wanawake kiuchumi, ikiwamo kuweka sera madhubuti na maboresho ya mfumo wa bajeti unaopunguza idadi ya wanawake na wasichana wanaoishi katika umasikini.

Ameiambia Redio UN News Kiswahili baada ya kumalizika mkutano unaohusu usawa kijinsia, akifafanua ni safari ndefu, ila mwelekeo upo.

Mkuu huyo wa nchi wa kwanza mwanamke tangu kupatikana uhuru, anasema hoja ya jinsia ilianza kupigiwa kelele zama za Rais Jakaya Kikwete, akirejea Bunge la Katiba na dhana iliyoibuliwa '50 kwa 50.'

Anatoa mfano, bunge la sasa wanawake wako asilimia 38, lakini lililopita lilikuwa asilimia 34 hadi 35.

"Kwenye Baraza la Mawaziri tulianza labda na asilimia 20, lakini mpaka uteuzi niliyoufanya karibuni, umetuvusha mpaka asilimia 36 na kazi inaendelea. Tutaweka wanawake wengi, pengine hatutafika '50 kwa 50', lakini tutasogea," anaeleza Rais Samia.

Pia, Rais Samia anasema kwa makatibu tawala wa mikoa kuna asilimia 46 wanawake na wanaume asilimia 54; wakuu wa wilaya wamekomea asilimia 38, akiwa na imani idadi itavuka kabla ya uchaguzi ujao

Anaendelea: "Mimi nachukulia kwamba Tanzania tumepiga hatua kubwa. Kwa sababu kuwapo kwangu hapa kulianza na uamuzi wa makusudi kwamba kutekeleza ile 50 kwa 50."

**CHIMBUKO LAKE**

Rais Samia anarejea mzizi wake, ulianzia ngazi ya bungeni kwenda chini kama vile madiwani, lakini mwaka 2015 serikali na Chama Cha Mapinduzi (CCM) zikaanza kutekeleza kwenye ngazi za juu.

"Ndio maana tukaamua ikiwa rais mwanamume, basi Makamu wa Rais atakuwa mwanamke, akiwa Spika mwanamume, Naibu Spika atakuwa mwanamke," anaeleza.

Anasema ameteua wanawake katika nafasi za juu, kwenye Baraza la Mawaziri, ikiwamo kumuongeza Balozi Liberata Mulamula, hata ikafanya idadi ya wanawake kufika asilimia 21 ya mawaziri, kutoka asilimia 17 aliyoikuta.



Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA: MAKTABA.**

Tangu kupatikana Uhuru mwaka 1961, nchini hakujakuwapo wanawake katika nafasi ya Katibu Mkuu Kiongozi, Mwanasheria Mkuu, Waziri wa Ulinzi na taasisi nyingi nyeti za dola.

**JICHO LA JK**

Rais Mstaafu, Jakaya Kikwete anathibitisha hoja hizo akitoa mfano wanafunzi waliomaliza elimu ya juu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), wanawake 1,920 sawa na asilimia 46.6, kati ya 4,121

Kikwete, mhitimu na sasa mkuu wa UDSM, anasema katika mahafali ya 51 chuoni hapo mwezi huu: "Takwimu hizi zisipoelezwa, hatuwezi kujua kama tunapiga hatua kubwa sana kwenye usawa wa kijinsia hadi ngazi ya elimu ya juu, ambako wanafunzi wengi wa kike walikuwa hawafiki au kumaliza."

Anasema ni matunda ya kuandikishwa uwiano wa usawa kijinsia. Anaendelea: "Wanapoanza kidato cha kwanza wanakuwa sawa wote kadri muda unavyokwenda wanapungua sijui wanaendaga wapi?

"Huku ngazi ya chuo wanakuwa wachache. Lakini, sasa tunaelekea hatua ya '50 kwa 50' kwenye suala la jinsia katika elimu ya juu.,"

**UKUSANYAJI MAPATO**

Rais Samia anaeleza mikakati yake kukuza uchumi kitaifa alipokuwa mkutanoni katika Umoja wa Mataifa, ameeleza juhudi za serikali kukuza uchumi, licha ya magumu ugonjwa UVIKO-19.

Anasema, baada kasi ukuaji uchumi kushuka kutoka asilimia 6.9 hadi 5.4 na Tanzania sasa inajitihadi kuziinua sekta zilizoathirika na maradhi hayo, ikiwamo utalii na kuimarisha mazingira ya biashara, pia kuvutia uwekezaji.

Rais Samia alipohutubia makatibu wakuu na viongozi wa taasisi za umma Aprili mwaka huu, aliwapa darasa namna ya kujenga mazingira ya kukusanya mapato serikalini kwa hiari.

Mkuu huyo wa nchi, tangu kuingia madarakani amekuwa akisisitiza namna wawekezaji wanatakiwa kutunzwa kiuchumi, pia kuwa na mazingira sahihi, kwani kinyume chake wanaondoka kwenda kwingineko.

Rais Samia alipokuwa Marekani kushiriki mkutano wa UNGA 67, alikutana na wafanyabiashara wa nchi hiyo na kuwahimiza kuimarishwa biashara kati yao na Tanzania.

**NURU YA MAFANIKIO**

Sehemu ya mafanikio ambayo yameanza kuonekana kiuchumi, ni kuongezeka mapato serikalini katika mwaka uliopo wa fedha, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ikisema kati ya Julai hadi Septemba iliyopita, imekusanya Sh. trilioni 5.15, sawa na ongezeko la asilimia 17.4, ikilinganishwa na mwaka uliopita.

Mkurugenzi wa TRA Aphayo Kidata, anataja mafanikio ni zao la mwamko wa kulipa kodi kwa hiari, ulipaji malimbikizo na kuimarika uhusiano kati yake na walipakodi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Geoffrey Mwambe, akifungua mkutano na wadau wa sekta binafsi kujadili fursa za Fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19, anataja ni mafanikio ya ushirikiano wao na sekta binafsi.

"Umekuwa msimamo wa Rais Samia kuwa serikali iache miradi inayoweza kufanywa na sekta binafsi iifanye kwa sababu ndio sekta inayoweza kutengeneza ajira nyingi nchini," anaeleza, akigusia namna serikali na sekta binafsi zinaboreshea mazingira ya kuvutia wawekezaji

"Mfano mzuri sasa akaunti zote za wafanyabiashara zipo 'free', makusanyo ya mwezi uliopita yalikuwa Sh. trilioni 5.151 tofauti na robo tatu ya mwaka uliopita yalikuwa Sh. trilioni 4.386, watu wamelipa kodi kwa hiari na mapato yamekuwa yakipanda bila kutumia nguvu."

Mwenyekiti wa umoja wa Benki nchini na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, anaunga mkono kuwa utaongeza mzunguko wa fedha nchini.

"Hii ni historia kama miradi yote ya nchi itakwenda hivi kila mtu mtaani atakuwa na fedha, kodi zitaongezeka.

Benki zipo tayari kushirikiana na sekta binafsi. Pia, tupo tayari kutoa mikopo ya muda mfupi ili kusaidia utekelezaji wa miradi mbalimbali inayotolewa na serikali kwa sekta binafsi," anasema Nsekela.

Anasemai miradi iliyopo ya thamani ya Sh. Trilioni 1.3 ikipitishiwa kwa wadau wa sekta binafsi, kuna kiasi kikubwa kitakachosaidia kuongeza mzunguko wa fedha nchini.

Nsekela anashauri serikali ipitishe fedha za miradi kwenye benki, ili kuongeza mzunguko wake, badala ya kuzihifadhi kusubiri utekelezaji miradi.

# Rwanda yawakamata watu 4 kwa kujaribu kutorosha pembe za ndovu

**KIGALI,** RWANDA

JESHI la Polisi nchini Rwanda linawashikilia watu wanne waliokamatwa Kigali wakijaribu kutorosha pembe za ndovu zenye uzito wa kilo 45. Mzigo huo ulikuwa ukisafirishwa kupitia Rwanda hadi katika nchi za bara la Asia.

Kwa maelezo ya taasisi ya taifa ya upelelezi na makosa ya jinai RIB shehena ya pembe za ndovu zenye uzito huo wa kilo 45 zilikuwa zikisafirishwa kutoka mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo kwenda barani Asia.

Shehena hiyo ilisafirishwa katika gari lenye nambari za usajili wa kampuni ya umeme ya nchi za maziwa makuu, kwa kifupi SINELAC ambayo inazishirikisha nchi za Rwanda, Burundi na Kongo ikiwa na makao yake mjini Bukavu.

Miongoni mwa waliokamatwa yumo mwanadiplomasia wa Rwanda ambaye ndiye mmiliki wa gari hilo lililobeba shehena hiyo.

Hata hivyo, maofisa wa usalama wameomba majina yake yasitajwe wakati akihojiwa na vyombo vya habari.

Kwa mujibu wa maelezo ya msemaji wa taasisi ya taifa ya upelelezi na makosa ya jinai Dk. Thierry Murangira, wote wanne walikamatwa kwa nyakati tofauti.

"Hawa walikamatwa walipokuwa wakijaribu kuingiza shehena hii ya pembe za ndovu. Upelelezi wa awali unatuonyesha kwamba walinuia kuziuza pembe hizi katika mataifa ya Asia na hapa Rwanda ilikuwa ikitumiwa kama njia ya kupitia tu. Hizi pembe za ndovu hazikuibwa hapa Rwanda, isipokuwa ni njia tu ya wahalifu.

Kukamatwa kwa hawa washukiwa kunatoa taarifa kwa watu wengine wenye mipango kama hii kwamba Rwanda si salama kwa wahalifu wanaopora mali za nchi jirani," alifafanua Dk. Murangira.

Msemaji huyo wa taasisi ya upelelezi na makosa ya jinai nchini Rwanda alisema kwamba ushirikiano unaendelea kuwepo baina ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo na Rwanda kurahisisha kupunguza visa vya uhalifu ambavyo vimekuwa vikiripotiwa katika mipaka ya nchi hizo mbili.

Mapema mwezi Juni mwaka huu marais wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo na Rwanda walikutana mjini Goma mashariki mwa Kongo ambapo viongozi wa pande hizo mbili walitia saini makubaliano ya ushirikiano katika sekta mbalimbali, zikiwamo usalama na biashara.

Matokeo yake sasa ndege ya shirika la ndege la Rwanda, Rwandair inafanya safari za kila wiki katika miji ya Kinshasa, Lubumbashi na Goma mashariki mwa Kongo.

**DW**




Sehemu ya eneo ambalo kundi la Kiislamu la IS linadai kutekeleza mashambulizi ya Jumamosi iliyopita Jijini Kampala.

## Uganda kufungua shule baada ya kufungwa kwa karibu miaka miwili

**KAMPALA,** UGANDA

RAIS wa Uganda, Yoweri Museven, ametangaza kuwa shule zote nchini humo zitafunguliwa mwezi Januari mwakani, ikiwa ni miaka miwili tangu zifungwe kwa sababu ya janga la virusi vya Corona.

Rais Museveni alisema shule hizo zitafunguliwa bila kujali watu wangapi wamepata chanjo ya virusi hivyo.

Mpaka sasa takwimu zinaonyesha ni asilimia chache tu ya waganda ndio waliopatiwa chanjo, ingawa Rais Museveni alisema kutakuwa na dozi nyingi na za kutosha za chanjo hizo mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka.

Walimu wengi nchini humo wanadaiwa kuacha kazi na kutafuta kazi nyingine baada ya masomo kusimama kwa muda mrefu ili kuweza kukidhi mahitaji yao, huku wengine wakisema hawatarejea kufundisha tena.

**BBC**

## Marekani yalaani mapinduzi ya kijeshi Sudan

**WOSHNGTON D.C,** MREKANI

RAIS wa Marekani, Joe Biden, amelitaka Jeshi la Sudan kurejesha utawala wa kiraia haraka na kuwaachia wanasiasa inaowashikilia.

Alitoa wito pia wa kumalizwa kwa vitendo vya vurugu dhidi ya waandamanaji ambao wanaendelea kuandamana kwenye mitaa kupinga mapinduzi ya Jumatatu yaliyoongozwa na Jenerali Abdel Fattah al-Burhan.

"Ujumbe wetu kwa Mamlaka za Jeshi Sudan uko wazi: Watu wa Sudan lazima waruhusiwe kuandamana kwa amani na serikali ya mpito inayoongozwa na raia lazima irejeshwe," alisema Biden

Rais huyo wa Marekani anaungana na jamii za kitaifa zilizolaani mapinduzi hayo ya Sudan, ikiwamo Umoja wa Ulaya.

Alisema atasimama na watu wa Sudan kwenye mapambano yao ya amani dhidi ya Mapinduzi.

Mpaka sasa watu 11, wanadaiwa kuuawa katika maandamano ya kupinga utawala wa kijeshi, yanayoendelea karibu katika miji yote mikubwa nchini humo, hasa Khartou.

**BBC**

## Viongozi wa zamani wataka nchi tajiri kugawa chanjo zisizotumika kwa nchi masikini

**LONDON,** UINGEREZA

ZAIDI ya viongozi 160 wa zamani na watu wengine maarufu duniani wameitaka Uingereza na mataifa mengine yenye nguvu Magharibi kutumia ndege za kijeshi kusambaza dozi za ziada za chanjo kwa nchi zinazoedelea.

Wameonya kwamba, iwapo hatua hazitachukuliwa katika mkutano wa kilele wa G20 mwishoni mwa wiki hii mamia kwa maelfu ya maisha huenda yakapotea, wakati huu chanjo zilizopitwa na wakati zikiteketezwa.

Miongoni mwa viongozi hao ni maraisi wa zamani 36, mawaziri wakuu 30 wa zamani na watu wengine maarufu zaidi ya 100.

Wanasema nchi tajiri zimefanikiwa kuchanja karibu asilimia asilimia 70 ya watu wao, huku nchi nyingi masikini zimefanikiwa kuchanja asilimia mbili tu. Na kutoa wito wa kuondolewa mara moja utofauti huo wa usambazaji wa chanjo.

Ili kufanikiwa hilo, wanasema Uingereza, Marekani, Canada na Umoja wa Ulaya zinapaswa kutumia ndege za kijeshi mara moja ili kusambaza dozi milioni 240 za ziada kwa nchi zenye uhitaji mkubwa na zingine milioni 200 mwezi ujao.

Kuruhusu mamilioni ya dozi za chanjo kumalizika muda wake, ni jambo lisilokubalika wakati maelfu ya watu wanakufa na Corona kila siku katika nchi masikini.

**BBC**

## Hakuna ugaidi utakaofanikiwa Uganda - Museveni

**KAMPALA,** UGANDA

RAIS wa Uganda Yoweri Museveni, amesema kuwa hakuna uasi wa vijijini wala ugaidi wa mijini utakaofanikiwa.

Alisema hayo kufuatia mashambulizi mawili tofauti ya mabomu nchini humo mwezi huu.

Katika hotuba yake ya televisheni kwa umma, Museveni aliwataja wahalifu hao kuwa ni kupe wanaoshambulia raia wasio na silaha, ambao watasakwa na kutiwa nguvuni.

Kundi la ADF linaojinasibisha na kundi la kiislamu la IS linalaumiwa kwa mashambulizi hayo mawili.

IS limekiri kuhusika na shambulio liliotokea Oktoba 23, katika mji wa Kampala na kusababisha kifo cha mhudumu mmoja wa baa na kujeruhi watu wengine watatu.

Mlipuko mwingine kwenye basi lililokuwa linatoka Kampala kwenda magharibi mwa nchi hiyo, ulitokea Oktoba 25 na kwa mujibu wa Polisi mlipuko huo ulimuua mlipuaji wa kujitoa mhanga , aliyekuwa amelivaa bomu hilo.

Kundi la ADF lina historia ya kuendesha vitendo vya kigaidi mijini na kwa mujibu wa Rais Museveni, walihusika kwenye ulipuaji wa mabomu 30 mjini Kampala kati ya mwaka 1997 na 2001 na kuua zaidi ya watu 120.

**BBC**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

N THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO..... 2021
IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE AKIDA JACKSON MKEMWA
AND
IN THE MATTER APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY AMINA ELLY MGENI
GENERAL CITATION
(Rule 75 of Probate Rules)

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before 16/11/2021.
**Dated at Dodoma this 13/10/2021**

MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT

## KUPOTEA KWA VYETI



DELISA WILLIAM NGOWI anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0729-0006 kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia MSOLWA SEKONDARI mwaka 2016. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba S4692-0688 kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia ST. JOSEPH'S CATHEDRAL mwaka 2019. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi: DAR/URA/RB/515476/2021.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MOHAMEDI SAIDI NJAMA anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili MC 691 CHQ. Chassis namba LZL12pg2KHD61614. Engine namba HJ137FM119046164. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: TAN/MAR/RB/374689/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

ATHANAS STEPHEN KAUZENI anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T 259 BEA – SUZUKI JIMNY. Chassis namba JB33111808. Engine namba G13B611848. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: DAR/CHU/RB/518183/2021.

**GARI INAUZWA AINA YA VOLKSWAGEN TOUREG YA MWAKA 2004 NAMBA DDV RANGI NYEUSI. INATEMBEA NA IKO KWENYE HALI NZURI SANA. BEI NI TSH. 15,000,000/- PIGA SIMU NAMBA 0762 810 451.**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

KURUTHUM MUSTAFA MUNIS anatangaza kupotea kwa kadi yake ya gari yenye namba za usajili T 795 DQT – TOYOTA SPACIO. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: DAR/OST/RB/516465/2021.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KUITWA SHAURINI MDAIWA
(MCA/84)
Mahakama ya mwanzo ya KEREGE WILAYA YA BAGAMOYO
NDOA/TALAKA
MADAI NAMBARI 15 YA 2021
Mdai: HAPPYNESS DAVID
Anamdai
Mdaiwa: HABIHUDI FRANLEY.
Kwa: HABIHUDI FRANLEY – LUSHOTO TANGA
Kwa kuwa mdai/wadaiwa/ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba
KUJIBU MADAI YA 1. TALAKA 2. MATUNZO YA MTOTO 3. MAKAZI YA MTOTO

Kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya ALHAMISI tarehe 11/11/2021 saa 2:30 asubuhi/kwa kujibu madai hayo, na kwa kuwa siku ni kukatwa shauri hili ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote inazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angalia kama hukuhudhura/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama imepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama leo tarehe 28/10/2021.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO KEREGE BAGAMOYO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI
Kituo cha KINONDONI Mkoa wa DAR ES SALAAM
Usimamizi wa mirathi Na. 455/2021
KATIKA SHAURI LA MIRATHI LA MAREHEMU CATHERINE .R. MOHAMED WA MASAKI KATIKA
SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA BALUHI PHILIPO BUDIKA

**TANGAZO**

*(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)*

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 22 Mwezi 11 Mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia; Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 11 Mwezi wa 10 Mwaka 2021.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

MARY MWANDILE MKOKA anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T 288 CCL – TOYOTA RAUM. Kadi ya gari yenye namba za usajili T 372 DDZ – TOYOTA HARRIER. Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: DSM/PHQ/RB/29499/2021.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

NDUGU BONIFACE ANYASIME MWAMPANJA anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili T711DGQ aina ya IST Rangi Nyeupe yenye Chasis No. NCP600039333, Engine No.ZNZ-FE1298 Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi namba DOD/DOD/RB/516782/2021

## KUPOTEA KWA CHETI



SAUMU ADAMU ALLEY anatangaza kupotelewa na BASIC CERTIFICATE IN MARKETING No. BCMK0005558 Kilichotelewa na COLLEGE OF BUSINESS EDUCATION Mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa polisi: DOM/RB/11866/2021.

## ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPIES T.LTD & COURT BROKER

### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**TUTAFANYA MNADA TAREHE 30/11/2021 SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA NYUMBA VILIVYOPO MTAA WA KOTA MPWAPWA MJINI MALI YA HAMISI MAHIMBA BAADA YA KUSHINDWA KESI YA MADAI NO. 8/2021 YA NEEMA LUFITA. MNADA UTAFANYIKA MAHALI NYUMBA ILIPO.**

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0756900540/ 0713913150.**

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO
DISTRICT AT MOROGORO
PROBATE AND ADMINISTRATION
CAUSE NO 43 OF 2021

In the Matter of the Estate of the Late **MAISHA MAGANGA MSONGA**

**By 1. FYOSEFYAKWE MAISHA MSONGA**
**2. ………………………………………………**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 01 day of 11 ………2021
Dated at MOROGORO this 29 day of 10 ………2021

………………………………
**RESIDENT MAGISTRATE**
DISTRICT COURT
P.O. Box 660, Morogoro

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MULEBA
MKOA WA KAGERA
RUFAA NA. 40/2021

KALOLI JOSEPH ……………………MRUFANI
DHIDI YA
1. MAENDELEO KULWA
2. JOYCE KAFARASI ……………………WARUFANIWA
KWA:-
1. MAENDELEO KULWA
2. JOYCE KAFARASI

( POPOTE PALE WALIPO)
Mnaarifiwa kuwa Rufaa Na. 40/2021 imepangwa kutajwa tarehe 16/11/2021 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, J.K. Banturaki saa 2:30 asubuhi, mahali - Muleba (Mamlaka ya Mji Mdogo).

Hivyo, mnaamriwa kuhudhuria wenyewe/ wawakilishi wenu mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Msipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yenu na hukumu kutolewa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hili leo tarehe 15/10/2021.

21.
………………………………
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MULEBA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ISMAIL LUTENGANO KIBIKI anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T 666 CLL – ISUZU PICK-UP. Chassis namba NKR66EA710478. Engine namba 1NKFE369. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: MKB/RB/152/2021.**

## KUPOTEA KWA VYETI




MICHAEL DUMA anatangaza kupotelewa na vyeti vya chuo kikuu
cheti cha chuo kilichotolewa na chuo kikuu cha kilimo cha Sokoine SUA chenye namba AEA/D/2015/0041 Taarifa ya Polisi IRI/IRI/RB/458783/202 Cheti cha matokeo ya chuo chenye namba AEA/D/2015/0041 kilichotolewa na chuo kikuu cha kilimo Sokoine SUA. taarifa Polisi IRI/IRI/RB/458786/2021.

## PASSPORT IMEPOTEA



HALIFA ABDALLAH MOHAMED anatangaza kupotelewa na PASSPORT No. AB393125 iliyotelewa 18 January, 2016 na kuishia 17 January,2026.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: DOD/DOD/RB/455712/2021.

## KUPOTEA KWA CHETI



SAID MUHIDINI MBARAKA anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.2579/0077 kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia KIVINJE SEKONDARI mwaka 2020. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi: DAR/MAG/RB/517017/2021.

## THE REGISTRATION OF DOCUMENTS CAP. 117 DEEP POLL ON CHANGE OF NAME

BY THIS DEED, I the undersigned MKASI MOHAMED ATHUMANI phone No. 0773 239 535 Tanga,
TANGA. Do hereby absolutely renounce and abandon the use of my former name of MKASI MOHAMED MAKALO
AND
That the name MKASI MOHAMED ATHUMANI is from my KADI YA MPIGA KURA No. T-1001-4743-949-5 and MKASI MOHAMED MAKALO is from my National Identify card No 19741126-21110-00001-16 all refers to one person namely MKASI MOHAMED ATHUMANI.
AND
That in pursuance of such changes of name as aforesaid, I hereby declare that will be known at all times hereafter in all records, deed and instrument in writing and in all actions and whatsoever use and sign the said name of MKASI MOHAMED ATHUMANI my name as my date of birth in lieu of the said former name MKASI MOHAMED MAKALO and as aforesaid.
AND
And I do hereby authorize and request all persons to describe and address me by such assumed name of MKASI MOHAMED ATHUMANI.
IN WITNESS WHEREOF I HAVE hereunder signed mu assumed name of MKASI MOHAMED ATHUMANI in lieu of the relinquished name of MKASI MAKALO

SIGNED AND DELIVERED by the said
MKASI MOHAMED ATHUMANI
MKASI MOHAMED ATHUMANI
Who is known/identified to me by;

The letter being known AT Tanga in my presence this
614 day of OCT, 2021
BEFORME
NAME
SIGNATURE
ADDRESS

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO TANGA MJINI

## KUPOTELEWA NA KADI YA GAR

AMBATANA AFRICAN SAFARIS anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA LAND-CRUISER yenye namba za usajili T 716 AJR engine namba lhz0083214,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa ARU/ARU/RB/517676/2021

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HADITHI

# HADITHI

TOM alipooa alidhani kuwa ataishi kwa amani, furaha na kupata utulivu kama inavyokuwa kwa rafiki na wenzake wote waliofanya hivyo. Siku zote ndoa ni kusikilizana, maelewano, na anayeoa hupata furaha na heshima. Kinyume chake, kwake amekuwa ni misukosuko, mikosi na balaa. Badala ya kuwa ndoa yenye furaha, akajiingiza kwenye mtego hatari ambao hata baada ya kuufahamu, hakuweza kuutegua tena. Alichelewa. Ukawa ni mwanzo ni vilio, maafa na mtiririko wa mambo ya kushangaza.
Hebu pata kila nakala ya gazeti hili kufuatilia kisa hiki cha kushangaza na kusikitisha.

# Namsaka Mke Wangu-17

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

"Sasa uniachaje mpenzi? Tumeshamaliza mpango wetu. Wewe nipe nauli yangu ya kurudi kwetu Singida na ada yangu ya mwaka ya kwenye kusoma chuo cha urembo kama tulivyoahidiana."

"He mbona mapema hivyo?"

"Ndiyo, wewe si unakwenda Dar? Mimi hapa Moro natafutwa kama kipusa, nikionekana naweza kuuawa na Sam. Siwezi tena kurudia kazi ya uhudumu wa baa, wala kukaa hapa Moro. Na hii yote ni kwa sababu yako."

"Najua hilo mama."

"Unakumbuka nilikwambia kuwa nilikuwa nafanya kazi ile ili nicheze mchezo wa upatu, nilitimiza pesa ya ada, nakwenda kujiunga na chuo, nasoma huku nafanya kazi, nikihitimu naachana nayo."

"Ndiyo ni kweli. Na unakumbuka kuwa nilikwambia kuwa usifanye tena hiyo kazi?" Tom naye alimuuliza Tedi.

"Nakumbuka. Lakini si kwa sababu ya kazi hii na imekwisha, wewe si unarudi Dar kusubiria mambo yako na mkeo?"

Tom alicheka kicheko kifupi, halafu akamwambia "Kwani wewe hutaki kwenda Dar?"

"Kufanya nini ?"

"Si nilikwambia wewe umeshakuwa si mpenzi wangu tu. Ni mshauri wangu na rafiki yangu. Siwezi kuruhusu kukupoteza tena."

Tedi alimuangalia Tom kwa jicho la mshangao na mahaba kwa wakati mmoja.

"Mkeo je?" Akauliza.

"Alinitoroka."

"Anakusubiri umsamehe."

"Hata nikimsamehe siwezi kukuacha. Si unakumbuka tulisema utakuwa mke wa pili?" Tom alisema kwa utani.

"Unaruhusiwa kweli." Aliuliza halafu wote wote wakacheka.

"Tuache utani Tedi, si muda wote ni utani tu. Tunakwenda wote Dar, mengine tutajua baadaye."

****************************

Spidi ya basi ilikuwa kubwa kiasi kwamba abiria wote walikuwa kimya. Mawazo yalimpeleka mbali sana Tom. Akakumbuka jinsi alivyokuja Morogoro kumtafuta mkewe aliyemtoroka wiki moja baada ya harusi yao.

Ni wiki tatu ameishi Morogoro na kukutana na mambo mengi ambayo hakuyajua kabla.




**Kabla ya kupanda basi hilo, Tedi alimshauri Tom waipeleke simu ile kwenye ofisi za Jeshi la Polisi mkoa wa Morogoro ili Sam akamatwe kwa kosa la kutaka kutaka kuchapisha kuweka picha chafu za aliyekuwa mpenzi wake kwenye mtandao wa kijamii**

Tayari anajerea akiwa ameshajua kila kitu kuhusu mkewe. Ni kwamba alikuwa na bwana yake. Anaitwa Sam. Alikuwa amechelewa kumuoa. Walikaa naye zaidi ya miaka 10. Mwanamke akakasirika, akatimkia Dar. Ndipo yeye alipomuoa na kutangaza ndoa. Akakubali haraka kwani ndicho alichokuwa akihitaji. Sam alimtishia kuwa atamuanika. Ni kwa kuchapisha picha chafu mtandaoni. Ndiyo, alikuwa nazo kwa sababu walikuwa wapenzi. Kwa miaka ya karibuni, hasa huu wa utandawazi, kuna baadhi ya wapenzi kujirekodi wanapokuwa wamejiachia. Wakiwa kwenye maraha yao. Hii inasababisha mmoja anapokasirika, au kuudhiwa, anaweza kufanya kitu chochote kwa kumtisha mwenzake kuwa anaweza kuweka picha hizo mitandaoni. Ndicho kilichotokea.

Kwanza mkewe Farida hakuamini. Akaolewa. Sam hakukata tamaa. Akamwambia amtoroke haraka sana mumewe ndani ya siku saba, la sivyo aachia picha hizo. Farida akatishika na kumtoroka.

Akajisifu kwa mbini kali aliyofanya hadi kujua hilo. Ni kwa kumtumia msichana Tedi aliyemkuta kwenye baa ya mama Mwenda ambako mkewe Farida huwa anakwenda na mpenzi wake Sam.

Akakumbuka jinsi alipomtoa Tedi kutoka kwenye uhudumu wa baa hadi kuwa 'mpelelezi', kujirahishisha kwa Sam kwa ajili ya kupata ushahidi wa kwa nini mkewe alimtoroka na kurejea Morogoro. Na kwa nini yupo na Sam. Awali Tom mwenyewe alikuwa hajui kama Farida na Sam walikuwa wapenzi.

Hata picha za video ambazo Sam alikuwa anatishia kuziachia kwenye mtandao zilichukuliwa, zikiwa kwenye simu ya mkononi ya Sam, kutokana na akili kubwa ya Tom mwenyewe akishirikiana na Tedi.

Tedi ndiye alikwenda kumnywesha Sam bia aliyoiweka vidonge, ambavyo vilimlaza usingizi wa pono Sam na akachukua kila kitu kukipeleka kwa Tom.

Sasa anarejea Dar. Alikuja peke yake, wanarudi wawili. "Vipi mwenzangu mbona kama una mawazo sana?" Tedi alimshtua Tom.

Tom alitabasamu, lakini kwenye hali inayoonyesha kuwa ni kweli alikuwa amezama kwenye lindi la mawazo.

"Ushamkumbuka mkeo nini?"

"Wewe acha utani bwana. Unajua nilikuwa nawaza nini?"

"Enhee, unawaza nini?"

"Nilikuja peke yangu Morogoro, lakini tunarudi wawili."

"Unarudi na nani?"

"Na huyu anayeuliza swali kuwa narudi na nani?"

"Haikuwa na mafanikio. Ulimkuja kutafuta mkeo. Umempata, lakini hujarudi naye." Tedi alichombeza.

"Hapana, imekuwa ya mafanikio sana. Nilikuja kumsaka mke wangu. Nilikuwa sijui chochote. Lakini nimejua mengi ambayo yalikuwa nyuma ya pazia. Nimeona mengi, nimejifunza mengi. Ningerudi peke yangu, labda ningekuwa na mawazo sana, lakini ni kama Mungu amenipa zawadi."

"Zawadi gani hiyo?"

"Wewe."

Tedi hakujibu kitu alibaki anamuangalia Tom usoni, halafu anakwepesha macho yake. Anatabasamu, kabla ya kumpapasa kifuani.

Wakati wote huo walikuwa amekaa siti moja ya basi moja naarufu lililokuwa likitoka Moro kuelekea Dar es Salaam.

Ghafla ikaingia meseji kwenye simu ya Tom. Alimpa namba wakati akiondoka na kumwambia chochote kile ambacho atataka kumweleza basi atumie namba hiyo.

Wote wawili waliiona. Wote wakawa na shauku ya kuisoma kwa sababu ilitoka kwa mtu ambaye walikuwa na kikao naye. Mtu aliyewashughulisha. Mtu ambaye ndiye aliyemfanya Tom kwenda Morogoro. Farida.

Kabla ya kupanda basi hilo, Tedi alimshauri Tom waipeleke simu ile kwenye ofisi za Jeshi la Polisi mkoa wa Morogoro ili Sam akamatwe kwa kosa la kutaka kutaka kuchapisha kuweka picha chafu za aliyekuwa mpenzi wake kwenye mtandao wa kijamii.

Tom alipinga. Hoja yake ni kwamba aachane na hilo kwa sababu hata wao hawakutumia njia halali ili kuipata simu ile.

"Kumbuka kuwa mimi ndiye niliyepanga mchezo mzima. Na wewe ukautekeleza kwa vitendo. Tukipeleka huko tatizo la polisi watashukuru sana, lakini watataka kujua simu ile ilipatikana vipi. Yaani ilichukuliwa vipi kutoka kwa mwenyewe. Hapo ndipo watakapogundua kuwa ulimuwekea vidonge kwenye pombe mmiliki wa simu. Hilo ni kosa. kazi ya kumkatama Sam ilibidi ifanywe na polisi wenyewe. Kwa hiyo wewe twende tu Dar." Tom akakumbuka kabla ya kufungua meseji ya Farida.

Macho ya Tom na Tedi sasa yakawa mbele kusoma meseji iliyoonekana kuwa ndefu, ambayo imetokwa kwa Farida. Mke wa Tom ambaye mpaka sasa alikuwa mkewe kisheria, kwani hakuwa na talaka.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# OMOG AFUNGUKA MTIBWA BADO HAKIJAELEWEKA BARA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Joseph Omog, amesema yuko katika wakati mgumu kutokana na matokeo mabaya ambayo timu hiyo imeendelea kuyapata katika mechi zake za Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara ambayo inaingia katika raundi ya tano.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Omog alisema hafurahishwi na matokeo hayo na sasa wanajipanga vyema ili kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mechi zao zijazo.**

Omog alisema licha ya kutoanza vizuri katika mechi za ligi hiyo, bado ana imani ya kupata matokeo mazuri kwenye michezo inayofuata kwa sababu wachezaji wake wameanza kuanza kupata muunganiko bora wa kiufundi.

Kocha huyo alisema bado anaendelea 'kukisuka' kikosi chake ili kufikia malengo ya timu na ana matarajio makubwa ya kupata pointi tatu katika mchezo dhidi ya Dodoma Jiji FC utakaochezwa kesho Jumamosi.

"Ni mechi ngumu tunaenda kucheza kwa presha kubwa ya kutafuta matokeo mazuri, nina matarajio makubwa ya kufanya vizuri na kupata pointi tatu muhimu katika mchezo dhidi ya Dodoma Jiji FC", alisema Omog.

Aliongeza wachezaji wake wamekuwa na molari kubwa kuelekea mchezo huo na tayari ameyafanyia kazi upungufu ulioonekana siku za nyuma na sasa wataingia kuwakabili Dodoma Jiji kivingine.

Naye Msemaji wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru, aliliambia gazeti hili kikosi chao kinatarajia kuwasili jijini Dar es Salaam leo jioni kwa ajili ya kuwakaribisha Dodoma Jiji.

Kifaru alisema mchezo huo utachezwa kwenye Uwanja wa Uhuru baada ya uwanja wao wa nyumbani wa Jamhuri Morogoro kufungwa ili kupisha marekebisho.

"Tumeendelea kujiimarisha katika kila idara, ninaamini tutautendea haki uwanja wa Uhuru ambao kwa sasa ni uwanja wetu wa nyumbani, tumejiandaa kupambana ili kuwarejeshea fuhara mashabiki wetu," Kifaru alisema.

Mtibwa Sugar ina pointi mbili kwenye mechi nne ambazo wamecheza, imetoka sare mara mbili, ikilazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Geita Gold FC na suluhu moja dhidi ya 'Maafande' wa Tanzania Prisons.

Baada ya mchezo huo, Mtibwa Sugar itasafiri kuelekea Mbeya kuwafuata Mbeya City katika mechi ya raundi ya tano itakayochezwa Novemba 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini.




Mchezaji wa timu ya vijana ya Yanga (Yanga B), Samson Peter (kushoto), akiwania mpira dhidi ya nyota wa GSM kutoka Temeke, Jafari Gonga, katika mechi ya kirafiki iliyochezwa kwenye Uwanja wa Chuo cha Sheria jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Choki: Nitastaafia Twanga Pepeta

**Na Sabato Kasika**

MWIMBAJI nyota maarufu wa muziki wa dansi, Ally Choki, amesema amechoka kuzunguka katika bendi mbalimbali na sasa ameamua kutulia kwenye bendi ya Africans Stars 'Twanga Pepeta' ya jijini Dar es Salaam.

Choki aliliambia gazeti hili sababu mojawapo ya kufanya uamuzi huo ni umri mkubwa ambao anao na tofauti na alivyokuwa miaka ya nyuma.

Nyota huyo alitaja sababu nyingine ya kutulia katika bendi hiyo ni kutaka kupata nafasi ya kukaa karibu na familia yake.

"Bendi yangu ya mwisho ilikuwa ni Super Kamanyola ya jijini Mwanza, niliporudi nikaamua kukaa bila bendi, nikitafakari jinsi ya kuendeleza kipaji changu na sasa nimeamua kutulia," alisema Choki.

Nyota huyo ambaye kwa nyakati tofauti amewahi kuondoka na kurejea Twanga Pepeta alisema hatarajii kufanya hivyo tena na badala yake anatamani astaafu muziki akiwa ndani ya bendi hiyo.

"Nilijitahidi sana kupanua wigo wa ajira kwa vijana hasa wa fani ya muziki, lakini juhudi hizo hazikuzaa matunda na mimi pia umri unakwenda, hivyo sioni kwa nini nilazimishe jambo ambalo naona limeshindikana," alisema Choki.

## Biashara yatambia michuano ya CAF

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 3-0 ugenini dhidi ya Prisons, Kocha Mkuu wa Biashara United, Patrick Odhiambo, amesema mashindano ya kimataifa ya Shirikisho Afrika yamewasaidia kuwakomaza wachezaji wake na kuwapa uzoefu.

Odhiambo alisema matokeo ya ushindi wa mechi hiyo ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara iliyochezwa juzi yamechangiwa na majaribio waliyopata kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na kusimamishwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

"Nadhani michuano ya kimataifa imetupa uzoefu wa kujiamini sana, ndiyo maana tunaendelea kufanya vizuri," Odhiambo alisema.

Hata hivyo kocha huyo amelalamika mchezo wa kutumia nguvu zaidi waliokuwa wakicheza wapinzani wao.

" Wenzetu wamecheza mpira wa rafu sana. Wametupa majeruhi wengi. Unajua kuna maisha baada ya mpira, sasa walikuwa wanafanya kazi ya kurukia wachezaji wangu, si vizuri," aliongeza kocha huyo raia wa Kenya.

Biashara United inasubiri hatima yake ya kuendelea na mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika, baada ya kuandika barua ya kusogeza mbele mchezo wao wa marudiano dhidi ya Al Ahli Tripoli ya Libya kufuatia changamoto ya usafiri iliyowapata.

## JKU yaitangazia vita Black Sailor

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa Black Sailor, Salehe Machupa amesema timu yake imedhamiria kufanya vyema katika msimu huu tofauti na walivyokuwa wakati wanapanda daraja kucheza Ligi Kuu Zanzibar.

Black Sailor inatarajia kukutana na JKU katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan kuanzia 9:00 mchana.

Machupa aliliambia gazeti hili msimu huu wamejipanga vizuri kuhakikisha wanapata alama tatu muhimu katika mchezo wao wa kwanza ili kuwaweka wachezaji wao kwenye hali ya kujiamini.

Kocha huyo alikiri msimu uliopita hawakufanya vizuri kutokana na ugeni waliokuwa nao kwenye ligi hiyo pamoja na kutofanya usajili wa wachezaji wenye uwezo wa kuhimili ushindani.

Naye Kocha Mkuu wa JKU, Sheha Khamis, alisema timu yake ipo tayari kupambana na Black Sailor na wamejipanga kuanza vyema msimu mpya.

Mechi nyingine za Ligi Kuu Zanzibar zitakazochezwa leo ni kati ya Selem View dhidi ya Yosso Boys wakati Mlandege FC itaumana na Kisiwani.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### HAZARD AWEKWA SOKONI

CHELSEA na Newcastle United ni miongoni mwa timu za Ligi Kuu England zinazohusishwa na usajili wa Eden Hazard, 30, kutoka Real Madrid ifikapo Januari. ***(ESPN)***

### SARR ANUKIA NEWCASTLE

WAMILIKI wapya wa Newcastle wanammendea winga wa Watford, Ismaila Sarr, 23, mmoja wa wachezaji wa mwanzo kutaka kumsajili. ***(Mail)***

### DEMBELE KUIBEBA BARCA

MATUMAINI ya Newcastle United kutaka kumsajili mshambuliaji wa Barcelona, Ousmane Dembele, 24, yameongezeka baada ya kutakiwa kumlipa kocha wake wa zamani, Ronald Koeman pauni milioni 10 kama fidia. ***(Express)***

### SOLSKJAER MAMBO MAZURI

KLABU ya Manchester United itapaswa kumlipa Kocha, Ole Gunnar Solskjaer pauni milioni 7.5 kama itafikia uamuzi wa kumtimua raia huyo wa Norway. ***(Sun)***

### CONTE BADO SANA

MANCHESTER United huenda isimtumie kocha wa zamani wa Inter Milan, Antonio Conte kama mbadala wa Ole Gunnar Solskjaer kwa sababu ya gharama kubwa za kumlipa Mtaliano huyo. ***(Star)***

### WEST HAM KUUZA HISA

KLABU ya West Ham ipo kwenye mazungumzo na bilionea wa Jamhuri ya Czech, Daniel Kretinsky kuhusu uuzaji wa hisa asilimia 27 za klabu hiyo. ***(Sky Sports)***

### LUKAKU ALITAKIWA CITY

KLABU ya Manchester City ilijaribu kumsajili Mbelgiji, Romelu Lukaku, 28, kutoka Inter Milan mwaka jana kabla ya nyota huyo kujiunga na Chelsea hapo Agosti, mwaka huu, wakala wa mchezaji amesema. ***(Telegraph)***

### BARCA, ARSENAL VITANI

ARSENAL huenda ikakabiliwa na ushindani kutoka Barcelona kwenye mbio za kumsajili mshambuliaji wa Manchester City, Raheem Sterling. ***(Football.London)***

### TUCHEL ASAKA STRAIKA

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel ameuomba uongozi wa juu wa timu hiyo kusajili straika mwingine ifikapo Januari ili kumpunguzia mzigo, Romelu Lukaku. ***(Transfer Window Podcast via Express)***

### WARD-PROWSE AWINDWA

KIUNGO wa Southampton, James Ward-Prowse, 26, anawaniwa na Newcastle United katika uhamisho wa Januari, ingawa alisaini mkataba mpya nao. ***(Football Insider)***

### DE BEEK BADO YUPO

KIUNGO wa Manchester United, Donny van de Beek, 24, na mlinzi wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Eric Bailly, 27, wamehakikishiwa mustakabali wao kwenye klabu hiyo. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO, MPENZI WAKE WANATARAJIA MAPACHA

Wazazi wamefurahia ujio wa watoto hao ambao watamfanya straika huyo kufikisha...

**MANCHESTER,** England

NYOTA wa Manchester United, Cristiano Ronaldo na mpenzi wake, Georgina Rodriguez wanatarajia watoto mapacha.

Wapenzi hao walitangaza habari hiyo kupitia kwenye ukurasa wao wa Instagram, wakisema: "Tunafurahia kutangaza kwamba tunatarajia mapacha. Mioyo yetu ina mapenzi makubwa - tunasubiri kwa hamu mapacha wetu."

Georgina amezaa na Ronaldo mtoto wa kike, Alana mwenye umri wa miaka mitatu, huku pia nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Ureno ni baba wa Cristiano Jnr (11), na mapacha, Eva na Mateo wenye miaka minne.

**Katika tangazo lao hilo waliloliweka kwenye Instagram lilipata watazamaji milioni 16.7 kwa muda wa saa tatu tu.**

Ronaldo amefunga mabao sita katika mechi tisa katika michezo yote tangu ajiunge na Manchester United kwa mara ya pili, akiwasili hapo akitokea Juventus wakati wa dirisha la joto.

Hata hivyo, kiwango cha hivi karibuni cha mashetani hao wekundu kimekumbwa na sintofahamu baada ya kushinda mechi tatu na kupoteza michezo mingine mitano katika mechi tisa walizocheza.

Jumapili iliyopita walitandikwa mabao 5-0 na Liverpool kwenye Ligi Kuu England na Kocha, Ole Gunnar Solskjaer akiwa kwenye wakati mgumu.

## HABARI MICHEZO

MECHI KALI
HOME
AWAY
TOTTENHAM
1.44 | 4.35 | 6.73
MANCHESTER UTD

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 619

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MARTINEZ ATIA SAINI MKATABA MPYA INTER



**MILAN,** Italia

STRAIKA wa Inter Milan, Lautaro Martinez ametia saini mkataba mpya wa miaka minne, klabu hiyo inayoshiriki Ligi ya Serie A imetangaza.

Mkataba huo mpya wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina utamalizika msimu wa 2025-26 na hakuna kipengele cha bei ya kununuliwa, kwa mujibu wa ripoti.

Martinez awali alikuwa akihusishwa sana na mpango wa kujiunga na Barcelona, huku pia kulikuwa na uvumi kuhusu kutakiwa na na klabu za Ligi Kuu England, Arsenal na Tottenham zilitajwa.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 ameamua kujikita zaidi kwa mabingwa hao wa Serie A, ambao wamemfanya kuwa fowadi muhimu zaidi baada ya kuondoka kwa Romelu Lukaku aliyetua Chelsea.

Martinez alisema Inter: "Ninafuraha sana kuwa hapa na kubaki kwa muda mrefu. Nashukuru sana mashabiki wa Nerazzurri.

Habari za Martinez kusaini mkataba mpya zimekuja wakati Inter ikitangaza kupata hasara ta euro milioni 245.6 kwa msimu wa 2020-21.



# Neymar awataka PSG wamnunue Raphinha

**PARIS,** Ufaransa

NEYMAR ameripotiwa kuwa amewataka Paris Saint-Germain kumnunua winga wa Leeds United, Raphinha.

Mchezaji huyo wa zamani wa Rennes, tayari ana mabao matatu kwenye mechi nane msimu wa 2021-22 wa Ligi Kuu England na amejiimarisha kama kiungo muhimu wa kikosi cha Kocha, Marcelo Bielsa.

Kiwango cha Raphinha kinaripotiwa kuwavutia Liverpool, lakini majogoo wanaweza kukabiliwa na ushindani mkubwa wa kuwania saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24.

Taarifa zinataja kuwa Neymar amemfahamu na kupendezwa na staa huyo wakati walipokuwa pamoja na Brazil kwenye

mapumziko ya k
hivi karibuni na n
huyo wa PSG ana
anaweza kums
Leonardo kum
mtani wake.

Raphinha aliw
vuni mabao ma
kutoa asisti mbil
mechi tatu za a
izoichezea Brazil
uliopita, lakini P
natajwa wa
kumnunua fow
Everton, Richarlis

## HABARI MICHEZO



# ,207,580

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 30/10/21 | 17:00 | Watford vs Southampton | 3.11 | 3.41 | 2.27 |
| 02. 30/10/21 | 17:00 | Burnley vs Brentford | 2.80 | 3.20 | 2.60 |
| 03. 30/10/21 | 17:00 | Derby vs Blackburn | 2.57 | 3.16 | 2.71 |
| 04. 30/10/21 | 17:00 | Hull City vs Coventry | 2.87 | 3.11 | 2.47 |
| 05. 30/10/21 | 18:00 | Metz vs St Etienne | 2.59 | 3.34 | 2.64 |
| 06. 30/10/21 | 19:30 | Tottenham vs Manchester Utd | 2.79 | 3.38 | 2.49 |
| 07. 30/10/21 | 19:30 | Valencia vs Villarreal | 2.86 | 3.36 | 2.45 |
| 08. 31/10/21 | 15:00 | Angers vs Nice | 2.80 | 3.25 | 2.50 |
| 09. 31/10/21 | 16:00 | Cadiz CF vs Mallorca | 2.67 | 2.97 | 2.92 |
| 10. 31/10/21 | 17:00 | Bordeaux vs Reims | 2.43 | 3.19 | 2.94 |
| 11. 31/10/21 | 17:30 | Augsburg vs Stuttgart | 2.80 | 3.30 | 2.47 |
| 12. 31/10/21 | 19:30 | Aston Villa vs West Ham | 2.77 | 3.42 | 2.49 |
| 13. 31/10/21 | 22:45 | Roma vs AC Milan | 2.49 | 3.42 | 2.77 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAMOSI - 30 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 3093 | Rubin Kazan vs CSKA Moscow | 3.13 | 3.23 | 2.21 |
| 14:30 | 1702 | Leicester vs Arsenal | 2.44 | 3.40 | 2.80 |
| 14:30 | 3961 | Fulham vs West Bromwich | 2.03 | 3.37 | 3.42 |
| 15:00 | 4675 | Elche vs Real Madrid | 6.02 | 4.23 | 1.52 |
| 16:00 | 2047 | Atalanta vs Lazio | 1.93 | 3.85 | 3.55 |
| 16:00 | 3653 | Mtibwa Sugar vs Dodoma FC | 2.79 | 2.60 | 2.79 |
| 16:00 | 5067 | Sirius FK vs Malmo | 5.97 | 4.62 | 1.40 |
| 16:30 | 1345 | Union Berlin vs Bayern Munchen | 7.58 | 5.58 | 1.33 |
| 16:30 | 3724 | SC Freiburg vs Greuther Furth | 1.44 | 4.67 | 6.36 |
| 16:30 | 4553 | Bayer Leverkusen vs VfL Wolfsburg | 1.90 | 3.64 | 3.78 |
| 16:30 | 4773 | Borussia Dortmund vs FC Koln | 1.47 | 4.87 | 5.56 |
| 16:30 | 4778 | Arminia Bielefeld vs Mainz | 3.68 | 3.33 | 2.03 |
| 16:30 | 5019 | Spartak Moscow vs Rostov | 1.68 | 3.73 | 4.62 |
| 17:00 | 1255 | Swansea vs Peterborough | 1.67 | 3.63 | 4.90 |
| 17:00 | 1266 | Newcastle vs Chelsea | 7.63 | 4.82 | 1.39 |
| 17:00 | 1717 | Huddersfield vs Millwall | 2.46 | 3.10 | 2.85 |
| 17:00 | 2663 | Burnley vs Brentford | 2.63 | 3.18 | 2.73 |
| 17:00 | 2732 | Celtic vs Livingston | 1.15 | 7.10 | 14.79 |
| 17:00 | 2781 | Liverpool vs Brighton | 1.23 | 6.19 | 11.97 |
| 17:00 | 4056 | Manchester City vs Crystal Palace | 1.21 | 6.46 | 13.09 |
| 17:00 | 4327 | Dundee Utd vs St Johnstone | 2.61 | 3.05 | 2.75 |
| 17:00 | 5275 | Bristol City vs Barnsley | 2.31 | 3.21 | 3.02 |
| 17:00 | 5484 | Kilmarnock vs Queen of South | 1.55 | 3.98 | 5.25 |
| 17:00 | 5684 | Stoke City vs Cardiff | 1.94 | 3.30 | 3.84 |
| 17:15 | 3985 | Sevilla FC vs Osasuna | 1.53 | 4.00 | 6.40 |
| 17:30 | 3914 | PSV Eindhoven vs Twente | 1.30 | 5.30 | 8.04 |
| 18:00 | 3554 | Metz vs St Etienne | 2.54 | 3.34 | 2.69 |
| 18:30 | 5226 | BK Hacken vs Kalmar | 1.98 | 3.39 | 3.39 |
| 19:00 | 1234 | Porto vs Boavista | 1.19 | 6.52 | 12.84 |
| 19:00 | 3196 | St. Gallen vs BSC Young Boys | 4.53 | 4.13 | 1.63 |
| 19:00 | 3626 | Verona vs Juventus | 3.72 | 3.62 | 1.94 |
| 19:00 | 5189 | Eyupspor vs Ankaragucu | 2.16 | 3.43 | 2.90 |
| 19:00 | 5994 | FC Krasnodar vs Kryliya Sovetov | 1.57 | 4.13 | 4.92 |
| 19:30 | 2867 | Standard Liege vs Kortrijk | 2.03 | 3.50 | 3.36 |
| 19:30 | 3108 | Valencia vs Villarreal | 2.96 | 3.36 | 2.36 |
| 19:30 | 3115 | Eintracht Frankfurt vs RB Leipzig | 3.84 | 3.99 | 1.81 |
| 19:30 | 3432 | Tottenham vs Manchester Utd | 2.78 | 3.41 | 2.46 |
| 19:30 | 3679 | Panetolikos vs Olympiakos | 7.11 | 4.24 | 1.43 |
| 19:30 | 4409 | Kfco Wilrijk vs RFC Seraing | 2.47 | 3.31 | 2.72 |
| 19:30 | 5161 | PAOK vs Apollon Smyrnis | 1.20 | 6.35 | 11.90 |
| 19:30 | 5995 | FC Ingulets vs Veres Rivne | 2.24 | 3.09 | 3.04 |
| 19:45 | 5672 | Heracles Almelo vs Ajax | 12.80 | 7.09 | 1.16 |
| 21:00 | 1228 | GD Estoril vs Benfica | 6.90 | 4.44 | 1.42 |
| 21:30 | 1860 | FC Zurich vs FC Basel | 2.61 | 3.60 | 2.41 |
| 21:45 | 1382 | St Truiden vs Brugge | 5.33 | 4.05 | 1.56 |
| 21:45 | 4254 | Torino vs Sampdoria | 1.98 | 3.65 | 3.55 |
| 22:00 | 1132 | Barcelona vs Alaves | 1.35 | 5.14 | 8.08 |
| 22:00 | 2689 | Reading vs Bournemouth | 4.44 | 3.60 | 1.73 |
| 22:00 | 4796 | Lyon vs Lens | 1.67 | 4.16 | 4.46 |
| 22:00 | 5219 | AZ Alkmaar vs PEC Zwolle | 1.22 | 6.08 | 10.78 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# VARANE AREJEA KUIKABILI SPURS

**LONDON,** England

RAPHAEL Varane amerejea kujiunga na kikosi cha kwanza cha Manchester United katika maandalizi kuelekea mechi dhidi ya Tottenham Hotspurs, itakayokuwa kwenye wiki ya 10 ya mechi za Ligi Kuu England.

Beki huyu alishindwa kucheza mechi tatu zilizopita baada ya kupata jeraha alipokuwa katika majukumu ya kitaifa mapema mwezi huu.

Staa huyu alitarajiwa labda angerejea uwanjani hapo Novemba, lakini ameonekana uwanjani katika mazoezi na kikosi cha kwanza mapema kuelekea mechi ya leo Jumamosi. Nyota huyo, amecheza jumla ya mechi saba za Manchester United tangu alipowasili klabuni hapo akitokea Real Madrid msimu wa joto, mechi tano zikiwa za Ligi Kuu England.

Mashetani Wekundu wamekuwa na kipindi kigumu kwa wakati Varane alipokuwa nje ya dimba, wakiruhusu magoli 11, kwenye mechi za michuano yote, dhidi ya Leicester City, Atalanta BC na Liverpool.



# *Sergi kocha wa muda Barcelona*

**BARCELONA,** Hispania

SERGI Barjuan ametangazwa kuwa kocha muda wa Barcelona, baada ya Koeman kufungashiwa virago, mpaka pale atakapopatikana kocha anayeweza kuchukua mikoba iliyoachwa.

Taarifa iliyotoka jana ilisema, "Barcelona imemtangaza aliyekuwa kocha wa Barcelona B, Sergi Barjuan, kuwa kocha mkuu kwa sasa na atachukua majukumu yote ya uongozi na kiufundi kwenye timu ya wakubwa."

"Nafasi yake ya muda itakoma pale tu klabu itakapompata mrithi sahihi wa kuchukua majukumu ya yaliyoachwa na Ronald Koeman."

"Rais Joan Laporta amemtambulisha rasmi Barjuan kwenye timu ya wakubwa jioni ya jana (juzi), kabla ya mazoezi kuanza kwenye Uwanja wa Ciutat Esportiva

Barjuan jana alihudhuria mkutano na waandishi wa habari, kuanzia majira ya saa saba mchana, kwenye ukumbi wa mikutano wa Ciutat Esportiva na kuzungumzia kuhusu mchezo, dhidi ya Alaves akiandamana na Laporta.

# Michezo

Jumamosi Oktoba 30, 2021
Nipashe




Ronaldo, mpenzi wake watarajia mapacha UKURASA 21




Kiungo wa Azam FC, Frank Domayo (kulia), akiwania mpira dhidi ya Mkenya, Keneth Muguna wa timu hiyo, wakati wakijiandaa na mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara dhidi ya Yanga itakayochezwa leo usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

## Makocha wazungu waigombea Simba

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Simba umesema mafanikio waliyopata katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliopita yamekuwa 'chachu' kwa makocha mbalimbali kutoka Ulaya kutuma maombi ya kutaka kurithi mikoba iliyoachwa na Mfaransa Didier Gomez, imefahamika.

Hata hivyo, Simba imesema idadi ndogo ya makocha kutoka barani Afrika ndio wametuma maombi ya kuajiriwa na mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, aliliambia gazeti hili jana wamepokea maombi 73 na idadi kubwa ya makocha waliotuma maombi yao wanatoka Ulaya.

Barbara alisema umefika wakati makocha kutoka hapa Afrika kujiamini na kujiweka tayari kukabiliana na changamoto ya kazi hiyo wanayoifanya.

Kiongozi huyo alisema hadi kufikia jana mchana asilimia 95 ya maombi waliyopokea yanatoka kwa makocha walioko nje ya Afrika.

"Inaonekana ama makocha wetu wanaogopa kukutana na changamoto ya ushindani au hawana sifa za kutosha kutuma maombi," alisema Barbara.

Aliongeza hii ni dalili kwamba umefika wakati wa kila klabu kuweka vigezo vya aina ya kocha inayemhitaji kwa ajili ya kuwa tayari kukabiliana na ushindani lakini pia kufikia malengo ya kufanya vyema kwenye michuano ya kimataifa.

Kwa sasa Simba iko chini ya Thierry Hitimana na katika mchezo wake wa kwanza baada ya kukabidhiwa mikoba alifanikiwa kuifunga Polisi Tanzania bao 1-0 na kesho atakiongoza kikosi hicho kuwakaribisha Coastal Union kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

# Yanga yatamba kuipoteza Azam

**Na Saada Akida**

## ●●● Yasisitiza iko kamili kuendeleza dozi kwa...

MBIO za kuwania ufalme wa soka nchini zinatarajia kuendelea tena kwa Yanga kuwakaribisha Azam FC katika mchezo wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

**Mbali na kila timu kuhitaji pointi tatu muhimu, mechi hiyo pia itakuwa ya kulinda heshima na kuweka rekodi mpya kwa timu hizo kwenye ligi hiyo.**

Rekodi zinaonyesha timu hizo zimekutana mara 26, Yanga ikiwa imeshinda mechi 10 huku Azam FC ikitoka kidedea mara nane na zikigawana pointi kwenye michezo nane.

Huu unakuwa ni mchezo wa pili kuwakutanisha makocha, Nassredine Nabi na George Lwandamina ambapo mara ya kwanza walipokutana, Azam Fc iliondoka kifua mbele kwa ushindi wa bao 1-0, shukrani kwa Prince Dube, aliyepachika goli hilo.

Akizungumza jijini jana, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema anaamini wanakutana na timu nzuri ambayo imetoka kuonyesha kiwango kizuri katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Kaze alisema Yanga imejipanga kutumia vizuri faida ya kucheza kwenye uwanja wa nyumbani ili kuibuka na ushindi na hatimaye kurejea katika uongozi kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16.

"Ligi Kuu msimu huu inaushindani mkubwa lakini sisi kama timu kubwa tunaenda kushinda mchezo huu ambao ni muhimu kwetu kwa ajili ya kuendelea kujiimarisha na michezo itakayofuata. Vikosi vyote vimebadilika, hivyo watu watarajie mchezo wenye upinzani," alisema Kaze.

Naye Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, alisema wamejiandaa kuibuka na ushindi kutokana na maandalizi mazuri waliyofanya kulingana na ukubwa wa mchezo husika.

"Tumejipanga vizuri kuhakikisha tunapata matokeo mazuri, tutaendelea kumkosa Price Dube licha ya kuanza mazoezi, nina imani tuko vizuri na tunaenda kupambana kutafuta ushindi," alisema Vivier.

Aliongeza msimu huu wamedhamiria kutwaa ubingwa na tayari wameshafanyia kazi upungufu uliojitokeza kwenye mechi zilizopita.

"Tumeimarika, tumesahihisha makosa yetu na kesho (leo), tutaingia uwanjani tukiwa imara zaidi, kila mchezaji anafahamu umuhimu wa kupata matokeo mazuri katika mechi hii, tunajua haitakuwa mechi rahisi kwa kila upande," kocha huyo aliongeza.

Wakati huo huo, Kocha Msaidizi wa Mtibwa Sugar, Awadh Juma, amesema kikosi chao kimejiandaa vyema kimwili na kiakili kuwakabili Dodoma Jiji FC katika mechi ya Ligi Kuu itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini.

"Hivi sasa tuko kwenye kipindi cha mpito, tunaijenga Mtibwa mpya kwani tuna kocha mpya ambaye hawajui wachezaji vizuri. Tuna imani na wachezaji wetu licha ya kuwa tumepata matokeo yasiyoridhisha, kila mmoja ameona usajili wetu ulivyo, wakati utafika tutakaa sawa," alisema kocha huyo.

Kocha Msaidizi wa Dodoma Jiji, Mfaume Samata, alisema maandalizi ya mchezo huo yamekamilika na wao wataingia kuwavaa Mtibwa Sugar kwa heshima.

"Timu yetu iko kamili na hatuna mchezaji mwenye majeruhi, tunaingia katika mchezo huu tukihitaji pointi tatu ili tusogee juu kwenye msimamo wa ligi," Samata alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >